# Nipashe

Jumamosi Julai 3, 2021 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580630

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US


**Wataka** ripoti BoT iwekwe hadharani

UKURASA 3



SIKU 100 SAMIA IKULU

**Machinga** wafichua Rais alivyowaokoa dhidi ya manyanyaso

UKURASA 16



**Weeknd, Angelina Jolie kunani?**

UKURASA 14

# KESI YA SABAYA

• **Mahakama:** Sasa leteni ushahidi... *Endelea ukurasa 2*



Aliyekuwa Mkuu wa Wilaya ya Hai, Lengai Ole Sabaya (mwenye miwani), akijiandaa kupanda basi la Magereza kurudi mahabusu katika Gereza la Kisongo, baada ya mashtaka yanayowakabili likiwamo la uhujumu uchumi kuahirishwa hadi Julai 16, mwaka huu katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Arusha jana. **PICHA: ALLAN ISACK**

## YALIYOMO


UKURASA WA 4

**NSSF YATATUA KERO ZA WANACHAMA SABASABA**

MFUKO wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF), unatatua kero mbalimbali...

UKURASA WA 4

**KIGAMBONI YAKABIDHIWA VIWANJA 20,000**

WIZARA ya Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi, kupitia Ofisi ya...

UKURASA WA 7

**MBARONI TUHUMA ZA UTEKAJI, MAUAJI**

JESHI la Polisi mkoani Kagera linawashikilia watu wanne kwa tuhuma...


**Maombi mikopo HESLB rasmi**

UKURASA 2



Rais Samia Suluhu Hassan, akitoa heshima za mwisho katika jeneza lenye mwili wa aliyekuwa Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Barabara nchini (TANROADS), Mhandisi Patrick Mfugale katika viwanja wa Karimjee, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: IKULU**



# Rais Samia: Taifa limepoteza shujaa

• **Familia**, serikali wasimulia chanzo kifo cha Mfugale... *Endelea ukurasa 2*

**MICHEZO** **SIMBA, YANGA MWISHO WA UBISHI** UK.24 **MAONI, KATUNI** UK.6

# Maombi mikopo HESLB rasmi

**Na Mary Geofrey**

WAZIRI wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Joyce Ndalichako, amezindua mwongozo wa kuomba mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya juu kwa mwaka 2021/22.

Mwongozo huo umefunguliwa kuanzia jana hadi Julai 9, mwaka huu ili waombaji kuusoma na kuuelewa kabla ya kuanza kujaza fomu za kuomba mikopo.

Prof. Ndalichako akizungumza na waandishi wa habari jana jijini Dar es Salaam wakati wa kufuangua dirisha la mikopo kwa waombaji na uzinduzi wa mwongozo huo, alisema mwongozo unalenga kuwawezesha wanafunzi kusoma maelekezo ya namna ya kujaza fomu za mikopo.

Prof. Ndalichako alisema wanafunzi wengi wanakosa mikopo kwa sababu ya kukosea kujaza fomu zao na wale wanaowajazia fomu wanawachanganyia taarifa.

Kadhalika alisema kuna muongozo wa watoa huduma za intanenti ambao utatolewa kwa ajili ya kuwasaidia watoa huduma kuzingatia vigezo vyote vinavyotolewa na bodi ili wasiwakoseshe wanafunzi mikopo. "Kwa wanafunzi wanaoendelea kupata mikopo sipendi kuona wanachelewa kupata mikopo, sitapendelea kuliona hasa kupewa hela pungufu, wanafunzi wanatakiwa wapewe hela kamilifu ili wajikimu," aliagiza.

Alisema serikali imeongeza bajeti mikopo kutoka Sh. milioni 464 hadi bilioni 570, hivyo aliitaka Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB) kuhakikisha wanafunzi wote wanye sifa wananufaika nayo.

Mkurugenzi Mtendaji wa HESLB, Abdul-Razaq Badru, alisema wanatarajia kuwafikia wanafunzi 160,000 kutoka wanafunzi 149,000 walionufaika mwaka uliopita. Utoaji huo wa mikopo pia unashirikisha Shirika la Posta Tanzania ambao wana jukumu la kusafirisha maombi na kutoa huduma ya kujaza fomu na Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhamini (RITA) ambao hadi sasa wameshahakiki vyeti vya wanafunzi 50,028 kati ya wanafunzi 56,402 waliowasilisha maombi.

# Mahakama yaita mashahidi katika kesi ya Ole Sabaya

**Na Allana Isack,** ARUSHA

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Arusha, imeuagiza Upande wa Jamhuri kuhakikisha unawaandikia barua ya wito mashahidi kufika mahakamani kutoa ushahidi katika mashtaka mawili ya unyang'anyi kwa kutumia silaha yanayomkabili aliyekuwa Mkuu wa Wilaya ya Hai, Lengai Ole Sabaya na wenzake watano.

Hakimu wa Mahakama hiyo, Salome Mshasha, alitoa agizo hilo jana mahakamani huko baada ya kushindikana kusikilizwa kwa shauri hilo kutokana na Upande wa Jamhuri kushindwa kuwafikisha mahakamani mashahidi ili kutoa ushahidi.

"Hakuna haja ya kupoteza muda, kwa ufupi ninaagiza mashahidi waletwe na wafike mahakamani na tarehe ya kusikilizwa kwa shauri ipangwe bila ya kupoteza muda na tuache maneno mengi. Kwa kuwa ninyi ni wanasheria, mnafahamu sheria zinasemaje," Hakimu Salome aliagiza.

Akizungumza mahakamani huko, Wakili wa Serikali, Tarsila Gervas, alidai shauri hilo lilikuwa mbele ya mahakama hiyo jana kwa ajili ya kusikilizwa, lakini shahidi wa Upande wa Jamhuri alishindwa kufika mahakamani.

Kutokana na kutokuwapo kwa shahidi huyo, Wakili Gervas aliiomba mahakama kupanga tarehe nyingine ya kusikilizwa kwa shauri hilo la jinai namba 66.

Mawakili watano wa Upande wa Utetezi, Dankan Oola, Mosses Mahuna, Silvestar Kahunduga, Fredoline Gwemelo na Geston Justine, walidai wanataka waelezwe mahakamani idadi ya mashahidi ambao Upande wa Jamhuri umeandaa.

"Ikikupendeza Mheshimiwa Hakimu, kama tungeambiwa kuna mashahidi wawili au watatu siku ile ya kwanza, cha kushangaza sasa hivi mashahidi ndiyo wanatafutwa kwa njia ya kuiomba mahakama kuandikiwa barua ya wito wa kufika mahakamani kutoa ushaidi. Hii ina maana gani?

"Kwa kuwa kesi ilitakiwa kusikilizwa kwa madai kwamba shahidi amepata udhuru, ninaomba tusianze kupotezeana muda mapema hivi.

"Sisi tulijiandaa kwa ajili ya kusikilizwa kwa kesi lakini tunaambiwa shahidi tuliyemtegemea amepata udhuru, inawezekana mtu mmoja kuikwamisha mahakama hii isifanye kazi.

"Kwa hiyo tunaomba wakati mwingine kitu kama hiki kisitokee na watueleze mashahidi wapo wangapi na kama wana uthibitisho," alidai Wakili Oola.

Wakili wa Serikali, Gervas, alidai namna ya kuwafikisha mahakamani mashahidi ni jukumu lao wenyewe wenye kesi, hivyo hawawezi kuelekezwa siku ya kuwapeleka mahakamani.

"Nimesikiliza malalamiko na madukuduku ya mawakili wa upande wa utetezi kuhusu Jamhuri kushindwa kumleta shahidi mahakamani.

"Pia ninapenda kuiambia mahakama yako kuwa tumesikiliza hoja zao na wakati mwingine tutawaleta mashahidi hao, lakini namna gani ya kuwaleta ni jukumu letu kwa kuwa sisi ndiyo wenye kesi na hata tukiwa nao 20, hawawezi kutuelekeza tuwalete wote kwa siku ambayo wanataka wao kwa kuwa suala la haki ni la pande zote mbili," alidai Gervas.

Hakimu Salome baada ya kusikiliza hoja za pande mbili, aliahirisha shauri hilo hadi Julai 16, mwaka huu litakapokuja kwa ajili ya kusikilizwa kwa ushahidi wa Upande wa Jamhuri.

Katika hatua nyingine, mahakama hiyo ilisikiliza shauri la uhujumu uchumi linalomkabili Ole Sabaya na wenzake.

Katika kesi hiyo aliunganishwa na washtakiwa wengine wawili ambao ni mshtakiwa namba sita, Jackson Macha (29) na wa saba Nathan Msuya (31), wote wakazi wa Moshi mkoani Kilimanjaro.

Jana, ilikuwa mara ya tatu kwa Ole Sabaya na wenzake kupandishwa kizimbani wakikabiliwa na makosa matano ya uhujumu uchumi, rushwa, kuongoza genge la uhalifu, utakatishaji wa fedha na unyang'anyi wa kutumia silaha.

Mbali na Ole Sabaya, washtakiwa wengine ni pamoja na msaidizi wake wa karibu Silvester Stanslaus, Enock Togolani, John Odemba, Daniel Gabriel na Waston Mwakomange.




Waziri wa Katiba na Sheria, Prof. Palamagamba Kabudi (kulia), akizungumza wakati wa uzinduzi wa sherehe za miaka 7 ya siku ya watetezi wa haki za binadamu Tanzania, mkoani Dar es Salaaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Rais Samia: Tumepoteza shujaa wa madaraja

**Na Christina Mwakangale**

RAIS Samia Suluhu Hassan, amesema taifa limempoteza baba wa madaraja, viwanja vya ndege, barabara na mtu muhimu mwenye uadilifu, shupavu na mhandisi hodari, kutokana na kifo cha Mhandisi Patrick Mfugale.

Jana wakati wa kuaga mwili wa aliyekuwa Mtendaji Mkuu huyo wa Wakala wa Barabara (TANROADS), Rais Samia alisema hadi umauti unamfika, alikuwa anaandaa michoro ya barabara za mzunguko jijini Dodoma.

Alisema Mfugale alimfahamu vizuri zaidi alipotembelea daraja la Kigongo-Busisi, akipewa maelezo ya kina na kwa kujiamini kuhusu ujenzi wa daraja hilo.

"Taifa limepata pigo kwa kumpoteza Mfugale, kila binadamu anapaswa kutumia kipawa alichopewa na Mungu kukitumia ipasavyo," Rais alisema.

Waziri wa Ujenzi, Dk. Leonard Chamuriho, alisema Mfugale aliugua ghafla wakiwa kwenye kikao na walilazimika kumpeleka Hospitali ya Benjamin Mkapa jijini Dodoma ilikothibitishwa amefariki dunia.

Alisema kuwa kwenye kikao hicho, mtaalamu huyo wa madaraja alitoa taarifa ya kujisikia vibaya na kuondoka kikaoni.

"Katibu Mkuu aliongoza kikao... majira ya saa tano asubuhi, Mhandisi Mfugale alimwambia Katibu Mkuu kuwa anajisikia vibaya, akaamua kwenda kupumzika ofisini kwake.

"Katibu Mkuu alipokwenda kumuona, wakati kikao kikiendelea, alimkuta mhandisi Mfugale ameketi katika kiti na alipoulizaa, akajibiwa na wasaidizi wake kwamba alipoingia aliomba aongezewe kiyoyozi.

"Katibu Mkuu aliamua kuandaa usafiri hadi hospitalini na uchunguzi mfupi walibaini amefariki dunia," alisema.

Mtoto wa Mfugale, Alex, alisema kwa niaba ya wenzake; Pendo, Aaro, Queen na Alice kuwa baba yao aliwafundisha kuwa na imani kwa Mungu.

Mdogo wa Mfugale, Erasto Mfugale, alisema ni pigo kwa familia na kwamba hawakupata taarifa dhahiri ya kilichotokea hadi kusababisha umauti huo kwa ndugu yao.

"Asubuhi alipokuwa anakunywa chai nyumbani kwake Dodoma niliongea naye, sasa kilichotokea kazini kwake sisi hatujui.

"Tumefika Dodoma tumeenda hospitali tumeona na kufuatilia nyaraka na kusema 'hatujui ugonjwa, mgonjwa alikuwa ameshafariki', hatukuelewa tulichanganyikiwa," Erasto alisema.

Mfugale alifariki dunia Juni 29, mwaka huu jijini Dodoma. Mbali na Rais Samia, viongozi wengine walioshiriki kuuaga mwili wake jana, ni pamoja na Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa na viongozi wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar (SMZ).

# Mikakati 9 yabainishwa kukuza uwekezaji

**Na Maulid Mmbaga**

WIZARA ya Uwekezaji nchini imebainisha mikakati tisa kuiwezesha sekta hiyo kupiga hatua kimaendeleo ikiwa ni moja ya jitihada za serikali za kukuza uchumi na kuongeza Pato la Taifa.

Akizungumza na Nipashe jana, Katibu Mkuu Ofisi ya Waziri Mkuu Uwekezaji, Prof. Godius Kahyarara, alisema miongoni mwa mikakati iliyowekwa ni kuongeza juhudi za kuhamasisha uwekezaji kwa kutumia mitandao ya kimataifa.

Pia, alisema wameongeza wigo zaidi wa kuhamasisha uwekezaji katika mataifa mbalimbali kwa kutumia vyombo vya kimataifa ili kufikia idadi kubwa ya wawekezaji.

"Kituo cha Uwekezaji nchini kina ushirikiano na vituo mbalimbali vikubwa duniani ikiwamo Dubai, Malesia, Ujerumani na Misri, ambavyo Tanzania inavitumia kutangaza bidhaa zake kutokana na kuwa na mashine kubwa zinazowasaidia kusambaza matukio ulimwenguni," alisema Kahyarara.

Mkakati wa pili ni kutumia ofisi za ubalozi zinazoiwakilisha Tanzania katika mataifa mbalimbali ambayo yana utaratibu wa kutafuta wawekezaji wa kimataifa kupitia Wizara ya Mambo ya Nje.

Alitaja mkakati wa tatu kuwa ni kuendeleza kufanya uhamasishaji wa kuita wawekezaji kwa njia ya mtandao, na kufanya mikutano ya kimtandao (zoom) kutokana na hali ya janga la corona linaloikabili dunia kwa sasa.

Kadhalika katika mkakati wa nne ni kuondoa urasimu, kwa kuwa na kifaa TIC kitakacho muwezesha mwekezaji kupiga simu na kuzungumza chochote, kufanya ufuatiliaji na kupokea maoni yatakayotuwezesha kujua ni wapi penye shida na kuifanyia kazi.

"Pia tunashirikiana na wenzetu wa TAKUKURU kufuatilia mambo ya Rushwa kwa vijana wetu wanaohusika na uwekezaji na katika hilo hakuna udanganyifu na vijana wetu wanajua hivyo wako makini na utendaji kazi," alisema Kahyarara.

Mkakati wa tano ni kuimarisha benki ya ardhi, ambayo Rais Samia Suluhu Hassan aliagiza itengenezwe na tayari wakuu wote wa mikoa na taasisi za ardhi, wameandikiwa barua na wanazifanyia tathmini, kuzipanga na kuzipa majina.

"Kila ardhi sasa hivi ina namba na (GPS code) yake pia inatafutwa ukubwa wake na uhalisia wake ili iweze kutumika kwa ajili ya wawekezaji wageni na suala hilo ni zoezi endelevu, katika kulikamilisha hilo tunashirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu Uwekezaji, Wizara ya Ardhi na Kituo vya Uwekezaji," alisema Kahyarara.

Mkakati wa sita ni kushirikiana na halmashauri ili kuhakikisha kuwa wanasimamia matumizi mazuri ya ardhi za uwekezaji, na mkakati wa saba ni matumizi ya TEHAMA ambayo yameanza katika mfumo wa kusajili vibali vya kazi kwa njia ya mtandao ili kurahisisha kazi na kupunguza muda unaotumika.

Mkakati wa nane ni kuweka mfumo ambao utamuwezesha mtu yeyote akiwa mahali popote kuingia katika mtandao na kufanya chochote kinachohusiana na uwekezaji ili kuchochea ukuaji wa sekta hiyo.

"Mkakati wa tisa ni kutumia kauli za viongozi katika kuwavutia wawekezaji kwa mfano Rais katika hotuba zake nyingi amekuwa akizungumzia uwekezaji, sasa kauli hizo tunazitumia kuwapelekea wadau na kuwaambia kuwa sasa hivi hii ni kauli ya mkuu wa nchi anasema anataka wawekezaji, kwa sasa maombi ni mengi na bado tunaendelea kuyachakata," alisema Kahyarara.

Pia alieleza kuwa wamejipanga kuzikabili changamoto zinazoweza kujitokeza katika sekta hiyo ili kuhakikisha kuwa miradi inayowekezwa nchini inakuwa na matokeo chanya kwa kuweka utaratibu maalumu wa ukaguzi wa miradi mara kwa mara kuhakikisha kwamba shida yoyote inayoweza kujitokeza wanaishughulikia kwa wakati.

Aidha, alisema Watanzania watarajie ongezeko la ajira, kwa kuwa kwa sasa serikali inaweka utaratibu kuwa uwekezaji unaofanywa lazima uwe na msukumo mkubwa wa utoaji wa ajira hasa kwa vijana nchini.

"Hadi sasa mafanikio makubwa ya serikali ya awamu ya sita ni kuvutia uwekezaji wa Dola za Kimarekani bilioni 1.67 na ajira 24,000 ndani ya siku 100. Ukilinganisha na uwekezaji wa Dola milioni 300 na ajira 5,000 kwa kipindi kama hicho mwaka jana, hii ni rekodi ya kujivunia kwani haijawahi kutokea," alisema Kahyarara.

Vile vile, alisema kwa sasa serikali imeweka mkakati ambao unaelekeza uwekezaji wowote unaofanyika nchini ni lazima uwanufaishe wazawa.

Pia Prof. Kahyarara alisema matarajio yao mengine ni kutanuka kwa wigo wa kodi, kwa kuwa masoko pamoja na mapato yataongezeka jambo litakalosaidia kuwa na wingi wa kodi.

Matarajio yao mengine ni kukuza ushirikiano kiuchumi na nchi za kikanda na nchi za dunia na kuwa hiyo itasaidia kukuza uchumi na pato la taifa kwakuwa kutakuwa na idadi kubwa ya fedha za kigeni.



Makamu wa Rais, Dk. Philip Isdor Mpango, akizungumza na Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia masuala ya wanawake (UN WOMEN), Dk. Phumzile Mlambo Ngcuka, baada ya kumaliza kuwasilisha ahadi za Tanzania katika Jukwaa la Kizazi Chenye Usawa, jijini Paris, nchini Ufaransa juzi. **PICHA: OMR**

# CHADEMA, Zitto wataka ripoti BoT iwekwe hadharani

**Na Romana Mallya**

BAADHI ya vyama vya upinzani vimeitaka serikali kuiweka wazi ripoti ya ukaguzi maalum uliofanyika Benki Kuu ya Tanzania (BoT) ambayo ilikabidhiwa kwa Rais Samia Suluhu Hassan, juzi mjini Dodoma.

Rais Samia alikabidhiwa ripoti hiyo kutoka kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), Charles Kichere, kama alivyoagiza uchunguzi ufanyike wa fedha zilizotolewa benki hiyo kati ya Januari na Machi, mwaka huu.

Wakitoa maoni yao baada ya kuzungumza na Nipashe jana kwa nyakati tofauti, baadhi ya viongozi wa vyama vya upinzani walitaka serikali iiweke hadharani ripoti hiyo.

Jumatatu ya wiki hii, Rais Samia wakati akizungumza na wahariri na waandishi wa habari wa vyombo mbalimbali aliahidi kuwa ripoti hiyo itatolewa.

Katibu Mkuu wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), John Mnyika alidai upo ukweli unaelekea kufichwa kuhusu ufisadi kwenye matumizi ya fedha za serikali.

"Badala ya taarifa fupi kwa vyombo vya habari iliyotolewa ni muhimu ripoti kamili ikawekwa hadharani. Taarifa ya kuwa kuna matumizi ya fedha yamefanyika mara mbili ilipaswa kuambatana na majina yao kuchukuliwa.

"Ikiwa ni uchunguzi wa kweli na wa kina utafanyika hakuna namna aliyekuwa mlipaji mkuu wa serikali na aliyekuwa Waziri wa Fedha watakwepa kuhusika na kashfa hii," Mnyika alidai.

Kauli ya kutaka ripoti hiyo iwekwe hadharani pia iliungwa mkono na Kiongozi wa Chama cha ACT - Wazalendo, Zitto Kabwe, ambaye alisema mpaka sasa ripoti hiyo wameiona kwa taarifa iliyotolewa kwa vyombo vya habari.

"Binafsi sijaisoma na mara nyingi huwa sitoi maoni kwenye jambo ambalo silijui, kwa hiyo ninachoweza kusema kwa sasa kwa kuwa Rais aliahidi kwamba ripoti hii itawekwa wazi basi iwekwe wazi ili tuisome na baadaye tuweze kutoa maoni, kwa sasa ni vigumu kuyatoa kwa sababu hatujui chochote kilichopo ndani ya ripoti hiyo," alisema.

Taarifa hiyo iliyopokelewa juzi na Rais Samia inatokana na agizo lake alilolitoa Machi 28, mwaka huu, alipopokea ripoti ya CAG kwa mwaka wa fedha 2019/20.

Katika taarifa ya ukaguzi maalum ambayo Rais Samia alipokea juzi, Kichere alisema ukaguzi uliofanyika umebaini fedha zilizotolewa BoT katika kipindi hicho zilifuata taratibu zote, isipokuwa baadhi ya malipo yalikuwa yanatoka Hazina Kuu kwenda katika taasisi mbalimbali za serikali yalibainika kuwa na upungufu.

Kwa mujibu wa taarifa hiyo, upungufu huo unajumuisha baadhi ya taasisi kama vile Wakala wa Barabara (TANROADS) na Mamlaka ya Bandari (TPA) kufanya malipo mara mbili kwa kazi moja au kuchelewa kutumia fedha zilizoidhinishwa kwa ajili ya malipo ya kazi husika.


THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
MINISTRY OF HOME AFFAIRS
IMMIGRATION DIVISION

Telegramu: IMMIGRATION
Telephone : 027-2751557
027-2752284
TeleFax 027-275228
REF. Na. IMM/MS/DN/16316/VOLI
MKUR UGENZI WA MAGAZETI MOSHI

THE OFFICE OF THE REGIONAL,
IMMIGRATION OFFICER ,
P.O.BOX 1049
MOSHI
KILIMANJARO
Date: 30/06/2021

**HII NI TAARIFA KUWA:**
**BWA GULSHAN KUMAR KEINTH**



Ambaye picha yake imeonyeshwa hapo juu,anaomba uraia kwa Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi .Yeye ni raia wa INDIA na Nchi atokayo ni INDIA.
Kazi yake /Shughuli zake ni Biashara, Anuani ya biashara zake BOX 488 MOSHI
Ameishi nchini tangu 1987, Pia amewahi kuishi Mkoa wa Kilimanjaro tu,
Mtu yeyeto mwenye sababu za kupinga mwombaji asipewe uraia, atume taarifa yake ya maandishi iliyosainiwa kwa:

KAMISHNA MKUU WA UHAMIAJI,
S.L.P 512,
DAR ES SALAAM.

FOR: REGIONAL IMMIGRATION OFFICER
KILIMANJARO

Kny: AFISA UHAMIAJI MKOA,
KILIMANJARO

116341802

# Kata yapoteza madiwani 2 mwaka mmoja

**Na Ahmed Makongo,**

MARA

DIWANI wa Kata ya Neruma (CCM), Halmashauri ya Wilaya ya Bunda, Michael Maungo, amefariki dunia akiwa nyumbani kwake Nundu, jijini Mwanza.

Diwani Maungo, alichaguliwa katika uchaguzi mkuu uliopita. Kata hiyo ilipoteza diwani wake, Isack Kabugu, ambaye naye alifariki ghafla akiwa nyumbani kwake.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Bunda, Charles Manumbu, alithibitisha kutokea kwa kifo hicho, juzi. "Mheshimiwa Maungo amefariki leo (juzi) wakati akiwa nyumbani kwake Nundu huko Mwanza," alisema. Manumbu alisema kuwa huyo ni diwani ni wa pili kufariki katika kata hiyo, mwezi Machi mwaka jana, aliyekuwa diwani wa kata hiyo na mwenyekiti wa halmashauri, Isack Kabugu, alifariki dunia ghafla wakati akiwa nyumbani kwake katika kijiji cha Kenkombyo.




Mkaguzi Mwandamizi wa NSSF, Revocatus Kiduli, akimwonesha mwanachama wa NSSF taarifa za michango yake, alipotembelea banda namba 13, katika maonesho ya Sabasaba. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# NSSF yatatua kero za wanachama 'chapchap' SabaSaba

**Na Mwandishi Wetu**

MFUKO wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF), unatatia kero mbalimbali zinazowakabili wanachama na wadau wake katika maonesho ya 45 ya Kimataifa ya Biashara SabaSaba, jijini Dar es Salaam.

Akizungumza na waandishi wa habari, Meneja Uhusiano na Elimu kwa Umma wa NSSF, Lulu Mengele, alisema katika maonesho hayo licha ya kutoa elimu ya hifadhi ya jamii kwa sekta binafsi na sekta isiyo rasmi, lakini wanatatua kero mbalimbali za wanachama wao.

Lulu alisema baada ya mabadilikoya Sheria ya Hifadhi ya Jamii ya mwaka 2018, sasa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii imebaki miwili; ambapo NSSF inahudumia sekta binafsi na sekta isiyo rasmi kama wakulima, wavuvi, wafugaji, wachimbaji na wajasiriamali wengine wote.

"NSSF tupo kwenye banda namba 13, tukifanyakazi ya pamoja ya hifadhi ya jamii, tunawakaribisha wanachama wetu wote waweze kutembelea banda hili ambapo inakuwa rahisi sana wanachama kuweza kupata huduma kutoka PSSSF au NSSF na tunawaahidi kero zao zote tunazitatua kwa haraka," alisema Lulu.

Alitoa rai kwa Watanzania wote wanaotembelea maonesho hayo, kufika katika banda la NSSF ili kupata elimu ya hifadhi ya jamii pamoja na kujiunga kwa ajili ya kujiwekea akiba ya baadaye.

Lulu alisema kila kitu kizuri kina changamoto, hivyo aliwakaribisha wale wanachama ambao wana kero mbalimbali watembelee katika banda hilo kwa kuwa ni sehemu ambayo kila huduma ataipata.

Naye, Bashiru Gwimile, ambaye ni mjasiriamali alisema alijiunga na NSSF kupitia sekta isiyo rasmi na anajiwekea akiba kila mwezi, alitoa wito kwa vijana wenzake kujenga utamaduni wa kujiwekea akiba kwa kuwa kuna faida nyingi ambazo watanufaika ikiwamo kupata pensheni ya uzeeni na mafao mengine yanayotolewa na NSSF.

"Nitoe wito kwa vijana wenzangu na Watanzania kwa ujumla tujenge utamaduni wa kujiwekea akiba kwa kujiunga na NSSF ili tutakapoishiwa nguvu za uzalishaji mali tuweze kunufaika na pensheni ya uzee" alisema.

Kwa upande wake, Afisa Mafao Mwandamizi wa NSSF, Stella Kabyemera, alisema kupitia maonesho hayo kero zote zinazowakabili wanachama na wadau zinapatiwa ufumbuzi wa haraka.

Alisema NSSF inatoa elimu ya hifadhi ya jamii, wanachama watapata fursa ya kuangalia taarifa za michango yao, wanachama ambao hawajapata kadi watazipata papo hapo kwa muda mfupi sana na watapata taarifa kuhusu uwekezaji.

# Kigamboni yakabidhiwa viwanja 20,000

**Na Munir Shemweta,** WANMM

WIZARA ya Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi, kupitia Ofisi ya Kamishna wa Ardhi mkoa wa Dar es Salaam, imekabidhi mradi wa viwanja 20,000 kwa halmashauri ya Manispaa ya Kigamboni, mkoani Dar es Salaam ili iweze kusimamia na kuendeleza eneo la mradi.

Hatua hiyo inatokana na agizo la Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, William Lukuvi, kutaka Manispaa ya Kigamboni kukabidhiwa mradi huo ili kutunza eneo hilo kwa mujibu wa mipango miji ya Wilaya ya Kigamboni.

Akizungumza wakati wa kukabidhi viwanja 20,000 jana, jijini Dar es Salaam kwa Mstahiki Meya wa Manispaa hiyo, Ernest Mafimbo, Kamishna wa Ardhi Msaidizi, Mkoa wa Dar es Salaam, Idrisa Kayera alisema lengo la kukabidhi mradi ni kutaka manispaa hiyo itunze eneo la mradi kwa mujibu wa mipangomiji na kuzuia uvamizi wa eneo hilo.

Kwa mujibu wa Kayera, awali, eneo la viwanja 20,000 katika manispaa hiyo kulikuwa na changamoto mbalimbali ikiwamo uvamizi wa maeneo ya wazi na kubainisha kuwa, kutokana na mamlaka ya upangaji kuwa chini ya halmashauri wizara imeona ipo haja ya kukabidhi mradi huo kwa halmashauri.

"Wizara imeona ikabidhi mradi huu kwa kuwa halmashauri ina nafasi nzuri ya kusimamia mipangomiji pamoja na kuendeleza miundombinu ambapo awali jukumu hilo lilikuwa likifaywa na wizara na tuzingatie mamlaka ya upangaji iko chini ya halmashauri," alisema Kayera. Maeneo ambayo mradi wa viwanja 20,000 upo katika halmashauri ya Manispaa ya Kigamboni unaohusisha viwanja 15,000 vilivyopo Gezaulole, Vijibweni, Muongozo, Kibada na Kisola.

Meya wa Manispaa ya Kigamboni, alitaka kuwapo kwa hati ya makubaliano ya mradi kati ya Wizara na Manispaa ya Kigamboni ili kuwa na ufanisi wakati wa usimamizi na kuendeleza mradi huo kwa maslahi ya wananchi wa Kigamboni. "Sisi tumefurahi kukabidhiwa huu mradi maana utatusaidia sana kama manispaa hata kupata mapato na tutautumia kwa maslahi ya Manispaa ya Kigamboni," alisema Mafimbo.

Mwenyekiti wa Kamati ya Mipangomiji kwenye Halmashauri ya Manispaa ya Kigamboni, Sanya Bunaya, ambaye ni Diwani wa Kimbiji alisema, pamoja na manispaa kupokea mradi huo, kuna wasiwasi wa kuibuka changamoto kutokana na kubadilika kwa msimamizi wa mradi na kushauri kuainishwa wazi kwa maeneo ya fidia na migogoro mingine ili manispaa ijue.

Hata hivyo, Kamishna Kayera alimtoa wasiwasi kuhusiana na suala la fidia katika maeneo ya mradi kwa kueleza kuwa suala hilo kama wizara walishalifanyia kazi kwa kuwa Wizara ya Ardhi ilipata mkopo kwa ajili ya wamiliki wote waliokuwa wakidai fidia na kusisitiza kuwa halmashauri ya Kigamboni inachotakiwa ni kuhakikisha maeneo ya mradi huo hayavamiwi na yanalindwa.

HABARI KITAIFA

# Kahawa Kagera kupata soko Ulaya

**Na Romana Mallya**

MAREKEBISHO mbalimbali yaliyofanyika katika kilimo cha kahawa yameliwezesha zao hilo linalozalishwa Wilaya ya Karagwe na Kyerwa, mkoani Kagera kupata soko nchi za Uswizi, Uingereza na Ufaransa.

Meneja Mkuu wa Chama cha Ushirika cha Wilaya za Karagwe na Kyerwa (KDCU), Oscar Mujuni, aliyasema hayo juzi wakati akizungumza na waandishi wa habari.

Mujuni alisema KDCU imeongeza tija ya uzalishaji wa kahawa baada ya kupata soko la uhakika la kimataifa kwa zao hilo kutoka kwenye wilaya hizo.

"KDCU tumefanikiwa kupata wanunuzi hawa kutokana na uamuzi wa kuzingatia ubora wa zao hili na sasa, tumeongeza imani kwa wanunuzi wa kahawa duniani ambao sasa wanaagiza kiasi kikubwa zaidi cha kahawa kutoka Tanzania," alisema.

Alisema uzalishaji na uchakataji wa zao la kahawa mkoani Kagera umepunguza kwa kiasi kikubwa ukosefu wa ajira kwa kuongeza idadi kubwa ya maelfu ya watu wanaojiajiri au kuajiriwa kwenye kilimo hicho.

"Mwaka 2017 kahawa iliyokuwa ikizalishwa iliuzwa na maganda yake ikiwa haina thamani kubwa na iliuzwa kwa mtu yeyote kwa sasa ushirika unaongeza thamani ya kahawa inayokusanywa kutoka kwa mkulima na kufikishwa viwandani ili kukobolewa na kupangwa kwenye madaraja na hii ndiyo iliyochangia wilaya hizi za Karagwe na Kyerwa kufika kwenye masoko ya kimataifa yakiwamo ya London, Uingereza na New York, Marekani," alisema.



Mwendesha pikipiki akiwa amebeba mzigo mkubwa wa mkaa na abiria akining'inia juu katika eneo la Sekondari ya Minaki, wilayani Kisarawe, mkoani Pwani mapema wiki hii, kitendo ambacho ni hatari kwa usalama barabarani. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Walinzi wasakwa tuhuma za wizi mgodini

**Na Marco Maduhu,**
SHINYANGA

JESHI la Polisi mkoani Shinyanga, linawasaka walinzi watatu wa kampuni ya Ndemuro Security, kwa tuhuma za kuiba mali katika mgodi wa almasi El- Hilali uliopo Mwadui Luhumbo, wilayani Kishapu.

Kamanda wa Polisi mkoani Shinyanga, George Kyando, akizungumza na waandishi wa habari jana, alisema tukio hilo lilitokea Julai mosi, majira ya saa saba usiku.

Aliwataja walinzi hao kuwa ni Jakaya Samweli, Benard Amos, na Enock Temelo, ambao wamedaiwa kuiba vifaa mbalimbali na mchanga viroba 30 udhaniwao kuwa na madini ya almasi.

"Tukio la kuibiwa mali za mgodi huu lilibainiwa na Meneja wa mgodi huo, Athony Mayeka, na walinzi hao walitelekeza silaha eneo la tukio aina ya shotgun mbili zenye namba za 41325, na nyingine namba 12, zikiwa na risasi tatu," alisema Kyando.

Alisema baada ya tukio hilo walikimbia kusikojulikana na jeshi la polisi linawatafuta ili kujibu tuhuma hizo.

Kamanda alitoa wito kwa wananchi mkoani Shinyanga, kutoa taarifa za uhalifu kwa jeshi hilo ili kuzuia.

# Wafanyabiashara kortini shtaka kusababishia NMB hasara mil. 365/-

**Na Hellen Mwango**

WAFANYABIASHARA watano, wakazi wa jijini Dar es Salaam, wamefikishwa mahakamani wakikabiliwa na mashtaka 14, ikiwamo kuwasilisha nyaraka za kughushi, kujipatia fedha kwa njia ya udanganyifu na kuisabishia Benki ya NMB hasara ya Sh. milioni 365.

Washtakiwa hao ni, Reginald Massawe (38), Gaston Danda (38), Cladius Kabwogi (34), Irene Marwa (25) na Noel Kitundu (34), wote kwa pamoja wamefutiwa kesi ya Uhujumu uchumi na kutakatisha fedha na kufunguliwa jalada la kesi mpya.

Mapema jana katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, iliyoketi chini ya Hakimu Mkazi Mwandamizi, Joseph Luambano, washtakiwa hao walisomewa mashtaka yao.

Upande wa Jamhuri ulidai kuwa, kati ya Desemba 2019 na Novemba 2020, jijini Dar es Salaam, washtakiwa waliongoza genge la uhalifu kwa kughushi, kuiba na kutoa utambulisho usio wa kwake.

Ilidaiwa kuwa, Mshtakiwa Massawe na Danda, Desemba 17, 2019 kwa nia ya kutenda kosa, walighushi maombi ya fomu ya benki na taarifa za huduma kwa mteja za benki ya ABC. Pia Masawe anadaiwa kughushi leseni ya biashara na cheti cha usajili wa malipo ya kodi kwa nia ya kuonyesha kwamba nyaraka hizo ni halali na zimetolewa na Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) huku wakijua kuwa siyo kweli.

Katika shtaka lingine, ilidaiwa kuwa, Desemba 10, 2019 katika benki ya NMB tawi la Msasani ndani ya Wilaya ya Kinondoni, mkoani Dar es Salaam, alijitambulisha kuwa yeye Riziki Kayenga na anafanya kazi TANESCO na kutumia nyaraka hizo kufungua akaunti yake binafsi huku akijua kuwa siyo kweli.

Jamhuri ulidai kuwa Septemba 30, eneo la Mlimani City, mshtakiwa Masawe kwa makusudi na kwa nia ya kutenda uovu aliwasilisha barua ya utambulisho kutoka TANESCO kwa dhumuni la kuonesha kuwa Kayenga ni mwajiriwa wa Shirika hilo na nyaraka hizo ni za halali wakati si kweli.

Aidha, inadaiwa washtakiwa hao wakiwa katika benki ya NMB eneo la Mlimani, wilayani Ubungo kwa njia ya udanganyifu walijipatia mikopo ya zaidi ya Sh. milioni 190 kwa njia mbalimbali kwa kubadilishana utambulisho wao.

Ilidaiwa kuwa, kati ya Desemba 2019 na Novemba 2020 jijini Dar es Salaam washtakiwa wote kwa njia ya udanganyifu waliisababishia benki ya NMB hasara ya Sh. milioni 360.

Washtakiwa wamekana mashtaka hayo na wamerudishwa rumande mpaka Julai 15, 2021.

Awali, Juni 29, mwaka huu, washtakiwa hao walifutiwa kesi ya uhujumu uchumi na mashtaka ya utakatishaji fedha na kisha kuwafungulia kesi ya jinai.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Mchezo Simba, Yanga uwe wa amani

**LEO** jioni mashabiki wa soka Afrika na kote duniani walioko Watanzania, watakuwa wakifuatilia mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara, mzunguko wa pili kati ya watani wa jadi Simba dhidi ya Yanga.

Ukiondoa kuwa ni mechi ya soka na utani wa jadi, ni moja kati ya mechi ya kitamaduni. Kwa sababu tofauti na nchi nyingi ambapo mashabiki hupenda timu kutokana na sehemu wanazoishi na hata 'dabi' zao huwa hivyo, Simba na Yanga zimeligawa taifa pande mbili kwa asilimia nyingi kama siyo zote.

Watanzania wengi kama hakuwa Simba, basi atakuwa Yanga, hata kama akionekana hapendi kabisa mambo ya soka, lakini ukikaa naye na kumdodosa kwa undani, utagundua ana nasaba ya moja wa klabu hizo kongwe kabisa na za kihistoria hapa nchini.

Simba na Yanga ni watani wa jadi na si mahasimu kama baadhi ya watu wanavyotaka kuwaaminisha wengine.

Asili ya klabu hizi mbali na huko nyuma kutumika kama sehemu za kujifichia kwa ajili ya kuwazuga wazungu, ili kufanya mikakati ya kujipatia Uhuru, lakini pia ni kutoa burudani, furaha, kujuana, kusaidiana na mengine yanayofanana na hayo.

Ndiyo maana wale hasa wanaofahamu asili ya utani huo, mmoja akishinda anawanunulia wenzake vinywaji, vyakula, matunda na vitu vingine vinavyofanana na hivyo kwa ajili ya kuwafariji.

Wakati huo aliyefungwa anakula huku akipokea maneno ya tambo na kujisifu kutoka kwa aliyeshinda.

Timu hizo zipo kwa ajili ya kutaniana na kuleta umoja na mshikamano, na upinzani wao unakuwa ni wa dakika 90 tu na si vinginevyo.

Kutokana na hali hiyo Nipashe tunawaomba waamuzi wanaochezesha mechi ya leo kusimamia sheria na kanuni zote za mpira wa miguu ili mechi iishe kwa wachezaji wa pande zote mbili kushikana mikono na kukumbatiana, huku waliopoteza waone kabisa kuwa walishindwa kimpira na si kwa sababu mwamuzi alichezesha ovyo.

Ukiangalia mechi nyingi ambazo wachezaji wanapaniana, kuchezeana rafu zisizo za kiungwana, kutupiana maneno makali, huanzishwa na waamuzi wanaoshindwa kuendana na kasi ya mpira, kutotafsiri vema sheria, lakini pia kuonekana kuegemea upande mmoja.

Upande mmoja unacheza rafu unaachiwa na kadi hazitoki, upande wa pili ukicheza mwamuzi anaonekana kukasirika na kutoa kadi kwa hasira, hii inafanya mpira uharibike.

Nipashe tunataka waamuzi watakaoacha alama, ili kesho badala ya mashabiki kumzungumzia vibaya mwamuzi, au mpira ulivyoharibika, wazungumzwe wachezaji waliocheza soka safi, waliofanya vizuri, waliofunga mabao na yeye mwenyewe kusifiwa kwa kuumudu mchezo.

Tunaamini kuwa timu itakayokuwa bora au kuwa mbinu sahihi ndiyo itakayoshinda na si vinginevyo.


Kwa upande wa wachezaji tunajua kuwa kila mmoja atakuwa amejipanga kwa ajili ya kutoa burudani.

Hii ndiyo nafasi ya wachezaji kuonyesha vipaji vyao halisi walivyojaaliwa na Mwenyezi Mungu, pamoja na ufundi na mbinu walizopewa na walimu wao, siyo kutuonyesha mpira ulio kama vita, ubishi, ulalamishi na rafu zisizo na kichwa wala miguu.

Nipashe tuaamini si tu Watanzania ambao watakuwa uwanjani pale Benjamin Mkapa, bali hata watu wa mataifa ya nje, wengine wakiwa wamesafiri kutoka nchi jirani kushuhudia mechi hiyo, hivyo tunataka soka safi na la ufundi ili watu waliolipa fedha za viingilio na waliolipia ving'amuzi vyao wafaidi na waone kuwa zimekwenda kihalali.

Simba na Yanga mwakani zote zinakwenda kucheza kimataifa, hivyo hii ni mechi ambayo inatakiwa kutoa sura ya kimataifa kuanzia kwa waamuzi hadi kwa wachezaji kuonyesha kuwa soka la Tanzania kwa sasa siyo lile tena, bali limepiga hatua. Tunazitakia kila la kheri timu zote mbili na mchezo mwema.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






Na barnabas Maro

## Muungwana Lazima Nilonge

# Dira ya binadamu...

**WAHENGA** walisema: "Dira ya binadamu ni kichwa." Walimaanisha kuwa kichwa cha binadamu ndiyo dira yake ya kumwongoza maishani.

Hii ni methali ya kutumiwa kwa mtu anayeelekea kutotumia akili katika mambo anayofanya na ambayo yanaelekea kutumiwa kwa kwenda upogo, yaani kuharibika.Ni methali ya kuzindua, yaani kumfanya mtu akumbuke jambo alilosahau: kitendo cha kumtoa mtu usingizini; amsha.

Gazeti maarufu la michezo nchini lilikuwa na maelezo mafupi kwenye safu ya "maoni ya mashabiki" yaliokuwa chini ya kichwa: "Leteni VAR." Iliandikwa; "NAIPONGEZA Azam Media kwa udhamini mnono katika Ligi Kuu, lakini nashauri watuletee na VAR ili kuondoa utata wa uamuzi unaoendelee kwenye Ligi yetu."

Katika safu ya "Muungwana lazima nilonge" ya gazeti hili unalosoma sasa, niliandika wazo kama hilo nikieleza jinsi baadhi ya waamuzi wa kandanda humu nchini wanavyotoa maamuzi yanayotofautiana na makosa yanayofanywa na wachezaji viwanjani! Wakati mwingine unaona mshambuliaji wa timu anafanyiwa kosa la wazi kwenye eneo la penalti lakini mwamuzi na mshika kibendera wake wanakuwa kama hawakuona tukio hilo. Hata wachezaji wa timu inayonyimwa penalti ya wazi wanapolalamika hawasikilizwi!

Kwa hali hiyo mchezaji anayelalamika sana huweza kutoa maneno machafu kwa mwamuzi na 'zawadi' yake huwa kuoneshwa kadi ama ya njano (yenye maana ya 'onyo la kwanza') au nyekundu kumtoa uwanjani!

Inapokuwa hivyo mashabiki wa timu inayonyimwa penalti hukasirika na kutoa maneno machafu kwa mwamuzi husika na mshika kibendera wake.

Kuna mawili: ama waamuzi hao wamepewa chauchau (rushwa) au ni wapenzi wa timu iliyofanya kosa hilo. Ieleweke kuwa haki ni jambo linalomstahikia mtu ilhali upendeleo ni tabia ya kufanya jambo kwa kumili yaani kitendo cha kitu au mtu kuelemea upande mmoja kimawazo au kimatendo; elemea. Kandanda, soka au kabumbu, ni mchezo unaochezwa kwa miguu, wenye timu mbili zinazoshindana. Watazamaji hutoa hela ili kwenda kuangalia mchezo huo hivyo huenda kuzishangilia timu wazipendazo ili zishinde. Huu ni mchezo unaopendwa na kuvuta watazamaji wengi zaidi kuliko michezo mingine duniani. Kwa hiyo ni mchezo unaotakiwa kuchezeshwa kwa kufuata sheria yaani taratibu maalum zenye vifungu mbalimbali zinazotungwa na chombo chenye mamlaka ya kusimamia taratibu za utekelezaji wa jambo fulani.

Shirikisho la kandanda humu nchini laitwa TFF (Tanzania Football Federation) ambalo sasa lataniwa kwa kuitwa "Tifua tifua." Ingekuwa vyema kama wangetafakari na kujiuliza ni kwa nini linaitwa hivyo! Wanaotoa fedha zao kuingia uwanjani hufanya hivyo ili kwenda kujiburudisha kwa hiyo wanataka haki itendeke kwani hao waitwao "Tifua tifua" nao hunufaika kwa fedha zinazotolewa na wanaoingia viwanjani.

Mwandishi aliyependekeza tuwe na VAR, aliishukuru Azam Media kwa udhamini mnono katika Ligi Kuu ya Kandanda nchini na kushauri ituletee pia VAR ili kuondoa utata wa uamuzi wa ovyo ufanywao mara kwa mara humu nchini, ama kwa waamuzi kutoona makosa au kuzipendelea baadhi ya timu wazipendazo ama kwa kupewa mlungula/mrungura!

VAR ni chombo kinachochukua picha za vitendo vyote vinavyofanywa na wachezaji uwanjani ili itokeapo kosa linalolalamikiwa na upande fulani, mwamuzi husimamisha mchezo na kwenda kwenye VAR iliyo pembezoni mwa uwanja kuangalia kinacholalamikiwa na moja ya timu inayolalamikia tukio linalolalamikiwa na timu isiyokubaliana na uamuzi wa refarii. Hapo mwamuzi hukubaliana na alichokiona kwenye VAR.

Kwa hali hiyo, nadhani suala la kuwa na chombo (VAR) uwanjani ni wajibu wa FAT sio Azam Media kama anavyopendekeza msomaji aliyeandika hivyo kwenye gazeti maarufu la michezo nchini. Kwa kuwa wanaolalamikiwa ni wateule wa TFF, basi wanaostahili kununua chombo hicho ni TFF yenyewe.

Wahenga walisema "Ushikwapo shikika (ukichwewa na jua lala). Maana yake unaposhikwa na mtu shikamana au jitahidi nawe. Methali hii yaweza kutumiwa kwa mtu aliyepatwa na tatizo kisha akapata mtu wa kumsaidia. Humhimiza ajikakamue au ajitahidi.

Ndo yale yasemwayo "Ushikwapo shikamana" (Ukichwewa na jua lala).Maana yake unaposhikwa na mtu nawe shikamana au jitahidi. Hii ni methali ya kutumiwa kwa mtu anayepatwa na tatizo kisha akapata mtu wa kumsaidia. Humhimiza ajikakamue au naye ajitahidi.

Kwa hiyo ni wajibu wa TFF kushughulikia ununuzi wa VAR badala ya kuitegemea Azam Media, TFF yaweza kupata fedha za kununua VAR kwa fedha zinazopatikana viwanjani na hata kuzishirikisha timu zinazoshiriki Ligi Kuu.

"Penye ni pana njia." Ikiwa mtu ana dhamira ya kufanya jambo hawezi kukosa njia, Hii ni methali ya kutumiwa kutukumbusha kwamba tuwapo na nia ya kufanya jambo lazima tutafanikiwa.

**marobarnabas@yahoo.com**
**0784 334 096**

HABARI KITAIFA



Meneja wa stendi ya mabasi yaendayo mikoani ya Msamvu, Manispaa ya Morogoro, Girbert Changalima (kulia aliyenyoosha mkono), akitoa maelezo kwa Mbunge wa Jimbo la Morogoro mjini, AbdulAziz Abood (katikati mwenye barokoa), kuhusu hali ya usafi kituoni hapo. Kushoto ni Kaimu Mkurugenzi wa Manispaa hiyo, Pilly Kitwana (mwenye kilemba). **PICHA: ASHTON BALAIGWA**

# Mbaroni tuhuma utekaji, mauaji

**Na Restuta Damian,** BUKOBA

JESHI la Polisi mkoani Kagera linawashikilia watu wanne kwa tuhuma za kuteka na kumuua kisha kumtupa ndani ya Mto Ngono, David James (35), mkazi wa Kijiji cha Katoro wilayani Bukoba mkoani Kagera.

Kamanda wa Jeshi la Polisi mkoani hapa, Revocatus Malimi, jana alithibitisha kutokea kwa mauaji hayo Juni 8, mwaka huu usiku.

Alidai kuwa kundi la watu waliojifanya askari polisi, lilikwenda nyumbani kwa marehemu kumkamata na kumpeleka kusikojulikana. Kamanda huyo alisema kundi la watu saba lilifika na kudai lifunguliwe mlango waingie ndani ndipo marehemu na mke wake, Erieth Zefrine (27), waliamka kwenda kufungua.

"Watu wasiopungua saba ambao baadhi yao walitambuliwa na mke wa marehemu, wakijitambulisha uongo kwa kujitaja majina ya askari polisi wa Kituo cha Kyaka wilayani Missenyi.

"Wakati anajianda kufungua, walivunja mlango na kumkamata na kuondoka naye.

"Kitendo hicho kilifanyika mbele ya mke wake na aliwatambua kuwa hawakuwa askari, bali wanakijiji wenzake na alitoa taarifa kwa ndugu zake, Polisi wa Kituo cha Katoro wilayani Bukoba. Baada ya kujua kuwa walitambuliwa walitoroka na kwenda kusikojulikana," alisema.

Kamanda Malimi alisema jeshi hilo lilianza msako kwa kushirikiana na wananchi na kufanikisha kupata mwili juzi Julai Mosi.

"Walikuwa wamemuua na walimfunga kamba aina ya katani miguu na mikono kisha kuzamisha ndani ya tinga tinga la maji ya Mto Ngono," alidai.

Kamanda Malimi aliwataja watuhumiwa hao wanaoshikiliwa kuwa ni Burchard Rwegasiray (67), Casto Rwegasira (27), Tuombe Elias (31) na Radius Mkuliusi (23), wote wakazi wa Kijiji cha Katoro.

Alidai sababu ya watuhumiwa hao kufanya kitendo hicho ni hisia zilizojengeka kuwa marehemu amesaliti kundi kwa kutoa siri ya shughuli walizokuwa wakishirikiana kuiba mifugo.

# Mbunge ataka kero mamalishe zitatuliwe

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

MBUNGE wa Morogoro Mjini, AbdulAziz Abood (CCM), amezuru katika Stendi Kuu ya Mabasi mkoani Morogoro (Msamvu) na kuitaka Manispaa ya Morogoro kuweka mazingira mazuri kwa wafanyabiashara wadogo.

Amesema wafanyabiashara hao bado hawana mazingira wezeshi kwao kufanya biashara kwa ufanisi unaozingatia usalama wa afya zao.

Mbunge huyo alitoa kauli hiyo juzi baada ya kupata malalamiko ya wafanyabiashara wadogo (machinga), wakiwamo mamalishe wanaojishughulisha na shughuli za biashara nje ya stendi hiyo, waliozuiwa kuuza vyakula vyao ndani ya stendi.

Akizungumza baada ya kutembelea maeneo mbalimbali yakiwamo ya mamalishe na maeneo ya vyoo vilivyopo ndani ya stendi hiyo, Abood aliitaka manispaa kuboresha mifumo ya vyoo na kuhakikisha maji yanapatikana kipindi chote ili kuepusha kujitokeza magonjwa.

Alisema stendi hiyo imekuwa ikipokea wageni wanaosafiri kwa mabasi kutoka mikoa mbalimbali nchini na nje ya nchi, hivyo suala la usafi na uwapo wa maji ni jambo muhimu nyakati zote ili kuepusha kutokea kwa magonjwa.

Mbali na kuhakikisha suala la kuweka hali ya usafi katika stendi hiyo, pia aliutaka uongozi wa Manispaa ya Morogoro kujipanga kukutana na makundi ya wafanyabiashara wadogo, wakiwamo mamalishe waliopo ndani ya stendi na nje, ili kufikiwa kwa mwafaka wa kuweka utaratibu wa kufanya biashara bila kusababisha kutokea kwa vurugu baina yao.

"Manispaa wekeni utaratibu wa wafanyabiashara wa vyakula, maarufu mamalishe wa nje, waelimishwe na kupangiwa utaratibu wowote utakaowawezesha kufanya biashara zao bila bugudha ndani ya stendi kwa kuwa wao ni sehemu ya ajira," alisema.

Mbunge huyo, akizungumzia machinga ambao wamelalamikiwa na Ofisa Afya wa Kituo cha Msamvu, Yamini Faraji, kuchafua mazingira katika stendi hiyo, alishauri uongozi wa stendi kukaa nao na kuwapatia elimu kuhusu madhara ya uchafuzi wa mazingira.

Abood pia aliitaka manispaa kupanga siku za kufanya usafi wa jumla katika stendi hiyo ambao unaweza kufanyika kabla ya kuanza kufanya biashara zao au baada ya kumaliza kufanya biashara hizo kwa lengo kuifanya stendi iwe katika hali ya usafi katika kipindi chote.

Kaimu Mkurugenzi wa Manispaa hiyo, Pilly Kitwana, alimpongeza mbunge huyo kutembelea stendi hiyo na kuahidi kufanyia kazi upungufu uliojitokeza, likiwamo suala la mamalishe na wafanyabiashara wadogo kuwekewa utaratibu utakaowezesha kuboresha kwa huduma ndani ya stendi hiyo.

# Madaktari wafundwa tathmini ya magonjwa

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

MADAKTARI na watoa huduma za afya 1,178 wamepatiwa mafunzo ya ujuzi wa kufanya tathmini za ulemavu uliotokana na ajali na magonjwa yatokanaya na kazi kupitia Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF) hadi kufikia Juni mwaka huu.

Mafunzo hayo yametolewa ili kuhakikisha huduma za tathmini za ulemavu uliotokana na ajali au magonjwa yatokanayo na kazi, zinawafikia walengwa huko waliko kwa haraka na kwa wakati.

Mkurugenzi Mkuu wa WCF, Dk. John Mduma, alibainisha hayo mjini Morogoro wakati wa mafunzo ya kuwajengea uwezo wa kufanya tahmini za ulemavu uliotokana na ajali na magonjwa yatokanayo na kazi kwa madaktari na watoa huduma za afya.

Alisema lengo ni kuongeza idadi ya madaktari na watoa huduma wa kufanya tathmini kutoka 1,085 na kufikia 1,178 nchi nzima.

"Lengo ni kuongeza mtandao wa wataalamu wenye ujuzi kwenye hospitali za umma na binafsi nchini kote ili kuondoa shida ya kuwafikia walengwa kwa muda na kwa haraka na hivyo kutoa tathmini stahiki na kwa wakati," alisema Dk. Mduma.

Mkurugenzi wa Huduma za Tiba na Tathmini wa WCF, Dk. Abdulsalaam Omary, akizungumza wakati wa kufunga mafunzo hayo, alisema yaliendeshwa na wataalamu kutoka WCF kwa kushirikiana na wataalamu wabobezi wa masuala ya tathmini za ulemavu.

"Tuna uhakika watakuwa wamefaidika sana na utaalamu huu ambao ni mpya kwao na kwetu sisi kama mfuko tumedhamiria kwa dhati kuhakikisha huduma zetu zinafika kila pembe ya nchi yetu na hivyo kurahisisha utoaji wa huduma kwa wafanyakazi watakaokuwa wamepatwa na matatizo hayo kazini," alisema.

Baadhi ya madaktari walioshiriki mafunzo hayo, walieleza jinsi walivyonufaika kwa kupata utaalamu na uelewa kuhusu masuala ya fidia na jinsi wanavyotakiwa kufanya kwa weledi tathmini kwa mtu aliyepata ulemavu uliotokana na ajali au magonjwa yatokanayo na kazi.

"Nitakuwa balozi mzuri kwa wataalamu wenzangu kwenye kituo changu cha kazi kwani nimeelewa kuwa tathmini za ulemavu uliotokana na ajali au magonjwa yatokanayo na kazi, itafanyika tu pale mgonjwa atakapokuwa amepona na kwamba hakuna tena tatizo litakaloendelea baadaye na siyo kabla," alisema Dk. Mohammed Khalifa kutoka Hospitali ya Wilaya ya Newala mkoani Mtwara.

Dk. Noel Saitoti kutoka Hospitali ya Ikenywa mkoani Dar es Salaam, alisema kabla ya kufika kwenye mafunzo hayo, licha ya kuifahamu WCF, hakuwa na uelewa zaidi wa majukumu ya mfuko huo.

## NARCO yataja mikakati kujiendesha kibiashara

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

MKUU wa Kampuni za Ranchi za Taifa (NARCO), Prof. Peter Msoffe, ametaja mikakati itakayosaidia kampuni hiyo kujiendesha kibiashara zaidi ili kutoa gawio kwa serikali.

Prof. Msoffe ameibainisha mikakati hiyo jana baada ya kumalizika kwa kikao cha makabidhiano ya ofisi na aliyekuwa Kaimu Meneja Mkuu wa NARCO, Masele Shilagi, kilichofanyika kwenye ofisi hizo jijini Dodoma.

Akizungumzia mikakati hiyo, Prof. Msoffe, alisema ni pamoja na kuifanya kampuni hiyo iwe kitovu cha umahiri wa masuala yote yanayohusu ranchi.

"Katika kuhakikisha hilo linafanikiwa ni lazima kampuni ijipange katika uzalishaji wa nyama ya kutosha iliyo bora, uzalishaji wa mifugo iliyo bora, kutoa mafunzo kwa wataalam na wafugaji, kujiendesha kibiashara na kuweza kupeleka gawio serikalini,"alisema.

Alisema ana matarajio makubwa kuwa hayo kutekelezwa kwa kuwa ameikuta kampuni ikiwa inaendelea kuimarika na kwa kushirikiana na viongozi na watendaji wa kampuni watatekeleza mikakati hiyo ambayo itawasaidia kutimiza azma ya serikali kwa kampuni hiyo.

Naye, Masele Shilagi, ambaye alikuwa Kaimu Meneja Mkuu wa Kampuni ya Ranchi za Taifa, alisema kampuni imekuwa ikiendelea kuimarika kimapato na kujiendesha bila kutumia ruzuku kutoka serikalini. Pia alisema amesimamia mapato na matumizi na kampuni kupata hati safi. "Kampuni imeweza kupima baadhi ya ranchi zake na kushughulikia migogoro iliyokuwapo ikiwemo ya uvamizi wa wananchi kwenye maeneo ya ranchi," alisema.

Aliwashukuru viongozi na watumishi wa NARCO kwa ushirikiano waliompatia kipindi cha uongozi wake na kuwaomba waendelee kutoa ushirikiano kwa Meneja mkuu mpya.

Naye, Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa Idara ya Uzalishaji na Masoko, Stephen Michael, alisema kuwa viongozi na watendaji wana wajibu wa kujipanga vizuri ili kuhakikisha malengo na matarajio ya serikali yanatimizwa.

"NARCO inazo fursa nyingi kwenye uzalishaji wa nyama bora, mifugo bora, malisho na utoaji wa elimu kwa wafugaji," alisema.

Alisema katika kuhakikisha fursa zinatumika na mapato yanaongezeka kama serikali ilivyopanga, ni lazima uongozi uone namna bora ya kushirikiana na sekta binafsi lengo likiwa ni kuongeza uzalishaji na kuongeza mapato.

# Serikali za Mitaa yatajwa kinara rushwa

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa nchini (TAKUKURU), mkoani Dodoma imesema sekta zilizoongoza kwa kulalamikiwa kwa vitendo vya rushwa ni serikali za mitaa ambayo ina asilimia 39, ikifuatiwa na ardhi ambayo ina asilimia 19.

Mkuu wa TAKUKURU mkoani Dodoma, Sosthenes Kibwengo, alitoa taarifa hiyo jana katika mkutano na waandishi wa habari uliofanyika jijini hapa.

Kibwengo alisema sekta nyingine ni za binafsi ambayo ina asilimia saba, elimu, afya na polisi zenye asilimia sita, kila moja.

Hata hivyo, aliwataka watumishi kwenye sekta zinazolalamikiwa zaidi kwa rushwa katika Mkoa wa Dodoma, kujitafakari kwa kuwa siku za mwizi ni arobaini.

Alisema pia wamefanya chambuzi sita za mifumo ya utendaji na utoaji huduma katika sekta za ardhi, elimu, mapato na ujenzi na mianya ya rushwa ilibainishwa.

"Baadhi ya chambuzi zilizofanyika ni rushwa na udanganyifu katika mitihani kwa baadhi ya vyuo na imebainika kuna baadhi ya wahadhiri na watumishi wengine wa vyuo wanashirikiana na wanafunzi kufanya udanganyifu katika mitihani," alisema Kibwengo.

Alisema uchambuzi wa mfumo wa kudhibiti mianya ya rushwa katika minada ulibaini zaidi ya asilimia 150 ya mapato kwenye minada hiyo yanapotea kwa njia ya rushwa.

"Wastani wa mapato yaliyokuwa yakipatikana kupitia mnada mmoja kwa siku ni Sh. 400,000, lakini ufuatiliaji wa TAKUKURU ulibaini kuwa wastani wa mapato halisi kwa siku ni milioni moja," alisema.

Kibwengo alifafanua kuwa wanaendelea kuwasisitiza wananchi kufatilia elimu wanazotoa ili kuyafahamu vizuri makosa ya rushwa kwa mujibu wa sheria ili kwa siku za usoni watoe taarifa zinazohusu vitendo vya rushwa.

Katika hatua nyingine alisema kuwa majalada 20 ya uchunguzi yalikamilika na mashauri mapya yalifunguliwa mahakamani.

"Uchunguzi wa taarifa zingine unaendelea ukiwamo wa watu ambao wameghushi nyaraka za umiliki wa eneo la hifadhi ya msitu wa Isabe lililoko wilayani Kondoa mahali ulipo mnara wa kampuni moja ya simu na hivyo kwa takribani miaka 12 wamejipatia Sh. milioni 70 kwa njia ya udanganyifu," alisema.

Alisema kitendo hicho ni kosa chini ya Sheria ya TAKUKURU sura ya 329 marejeo ya mwaka 2019.

Alisema tayari wamefanikiwa kumpata mtuhumiwa mmoja ambaye anaendelea kusaidia uchunguzi ili kuwapata wenzake na kwa sasa wamezuia malipo ya mnara huo ili kwa mujibu wa sheria yalipwe kwa mmiliki halali wa eneo ambaye ni Halmashauri ya Wilaya ya Kondoa.

Katika hatua nyingine alisema kuwa miradi 20 ya maendeleo yenye thamani ya Sh. 1,775,763,746 katika sekta ya elimu, afya na ujenzi ilikaguliwa kwa lengo la kujiridhisha iwapo thamani halisi ya fedha imepatikana kwa kuangalia iwapo kuna ufujaji.

Alisema miradi 19 imebainika kutekelezwa kwa kiwango stahiki, lakini wamebaini uchepuzi wa vifaa vya ujenzi vyenye thamani ya Sh. 41,850,000 kwenye mradi mmoja na wanafuatilia ili vifaa hivyo virejeshwe mara moja

"Ufuatiliaji wetu umewezesha kuokoa na kudhibiti jumla ya Sh. 215,660,000 ambazo zingepotea kwa kuchepushwa, kufujwa au kulipwa kwa watu wasio stahili kinyume nataratibu," alisema Kibwengo.

Alisema pia kuna gari la Ofisi ya Katibu Tawala Mkoa wa Dodoma ambalo baada ya kupata ajali lilipelekwa kwenye gereji na kwa kuwashirikisha wakala wa ufundi na umeme (TEMESA), ikabainika kwamba vifaa 101 vyenye thamani ya Sh. 87,785,000 vilichepushwa.




Naibu Spika, Dk. Tulia Ackson, akizungumza baada ya kukabidhi baiskeli maalum kwa watu wenye ulemavu kwa Mwenyekiti wa Jukwaa la Wanawake na Wasichana wenye Ulemavu Mtwara, Zamda Said Abdallah, wakati wa Mkutano Mkuu wa Uchumi na Mapendekezo ya Siku ya Mwanamke Mwenye Ulemavu Tanzania uliofanyika jijini Dodoma, jana. Kushoto ni Mwenyekiti wa Taasisi iliyoandaa mkutano huo ya Ikupa Trust Fund, Stella Ikupa. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Serikali yaagiza ukaguzi ununuzi taasisi za umma

**Na Saidina Msangi,** DODOMA

NAIBU Waziri wa Fedha na Mipango, Mhandisi Hamad Yusuff Masauni, ameiagiza Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma (PPRA), kuongeza kasi ya ukaguzi wa masuala ya ununuzi katika Taasisi za Umma ili kubaini upungufu na kuchukua hatua kabla ya kuisababishia serikali hasara.

Masauni alitoa agizo hilo jijini Dodoma alipokutana na kufanya mazungumzo na menejimenti pamoja na wafanyakazi wa mamlaka hiyo akiwa katika ziara yake ya kutembelea taasisi zote zilizo chini ya Wizara ya Fedha na Mipango.

Alisema, serikali inatumia kiasi kikubwa cha fedha kwenye ununuzi akitolea mfano bajeti iliyopita ya mwaka wa Fedha 2020/2021, Sh. trilioni 25 sawa na asilimia 75 ya bajeti yote zilitengwa kwa ajili ya kufanya ununuzi.

"Ili kudhibiti matumizi yasiyofaa ya fedha za Umma, ni lazima Idara ya ufuatiliaji na ukidhi ipatiwe wafanyakazi wa kutosha na wenye weledi ili ukaguzi ufanyike kwa ufanisi na kupunguza hasara kwa taifa," alisema Masauni.

Maelekezo ya Dk. Masauni yanakuja baada ya kuelezwa kuwa kutokana na changamoto ya uhaba wa watumishi katika Idara ya Ufuatiliaji na Ukidhi, PPRA inakagua wastani wa taasisi 120 katika taasisi 540 kwa mwaka.

Aliipongeza Taasisi hiyo kwa kusimamia mfumo wa ununuzi kwa njia ya mtandao ujulikanao kama TaNEPS, na kuagiza wataalam wa ndani wauboreshe ili kuhakikisha kuwa haitoi mwanya wa kutoa zabuni kwa watu wasio na vigezo na wanaotumia rushwa.

"Ni muhimu kuhakikisha kuwa mnapunguza uwezekano wa watumishi kukutana na wazabuni ana kwa ana ili kuepusha mazingira yanayoweza kuchochea rushwa na kuisababishia serikali hasara," alisisitiza.

Kwa upande wake, Kaimu Mtendaji Mkuu wa PPRA Mhandisi Mary Swai, alisema Mamlaka yake inakabiliwa na upungufu wa watumishi na kwa sasa ina watumishi 76 sawa na asilimia 48.

Alimshukuru Mhandisi Masauni kwa kuwatembelea kujua majukumu yao na kuahidi kuwa maagizo yote aliyowapatia yatafanyiwa kazi kikamilifu na kuendelea kufanya kazi kwa weledi na ufanisi mkubwa katika kuhakikisha kuwa sekta ya ununuzi wa umma inaleta tija na maslahi kwa taifa.





Spika wa Bunge, Job Ndugai (kulia), akisalimiana na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) mstaafu, Prof. Mussa Assad, baada ya kumalizika kwa sherehe ya Maadhimisho ya Miaka 60 ya ofisi ya CAG, jijini Dodoma jana. Katikati ni CAG Charles Kichere. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Ndugai aitaka ofisi ya CAG kuandaa ripoti utendaji watumishi serikalini

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

SPIKA wa Bunge Job Ndugai ametaka Ofisi ya Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali kujikita katika kuandaa ripoti za ufanisi ili kupata picha ya utendaji wa watumishi ndani ya serikali.

Ndugai, aliyasema hayo jana jijini Dodoma wakati alipokuwa akitoa hotuba yake kwenye maadhimisho ya miaka 60 ya ofisi hiyo toka kuanzishwa kwake.

Alisema, hivi sasa ipo haja kwa ofisi hiyo kuanza kujikita kuanda ripoti za ukaguzi wa ufanisi katika maeneo mbalimbali.

"Ni wakati sasa wa kuandaa ripoti hizi za kihasibu, lakini pia muanze kuandaa ripoti zinazohusu ufanisi ili kuondoa malalamiko yanayotoka kwa wananchi," alisema Ndugai.

Aidha, alisema kumekuwa na malalamiko kutoka kwa wananchi kuwa pamoja an ofisi hiyo kutoa hati safi, lakini kuna vitu vinaoneka kuwa haviko sawa.

"Wananchi bado wanalalamika unakuta halmashauri inapewa hati safi, lakini wakiangalia hakuna kitu ambacho kipo sawa hivyo ripoti hizi za ufanisi zitasaidia kuondoa malalamiko haya kwa kupima utendaji wa watumishi," alisema Ndugai.

Pia, alisema Bunge litaendelea kushirikiana na Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali katika kujadili ripoti zinazowasilishwa kwa maslahi ya taifa.

Alisema kuwa ripoti hiyo ni nyenzo muhimu kwa Bunge inayolisaidia kuhoji na kuisimamia serikali katika utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo.

"Pia tunaomba ofisi yako CAG, kuendelea kutoa elimu kwa waheshimiwa wabunge wetu ili kuwa na mbinu bora za kuhoji mambo mbalimbali katika maeneo yao na kuisaidia serikali yetu na rais wetu," alisema.

Kadhalika aliomba ofisi hiyo kutoa mafunzo kwa wahasibu hasa wa Ofisi ya Rais TAMISEMI ambao kwa kiasi wapo nyuma kutokana na kukosa mafunzo ya mara kwa mara.

"Mnaweza mkawa mnawahukumu wahasibu wetu kwa kufanya vibaya katika mahesabu, lakini ukweli ni kwamba wapo nyuma hasa wale wa TAMISEMI hawapati mafunzo ya mara kwa mara," alisema.

Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), Charles Kichere, alisema kuwa wanaishukuru serikali kwa kuendelea kuiwezesha kutekeleza majukumu yake kwa kuipatia fedha pamoja na rasilimali watu.

Vile vile, Kichere aliliomba Bunge kubadili muda wa kujadili ripoti yake anayoiwasailisha bungeni katika mwaka wa fedha husika tofauti na ilivyo sasa kujadiliwa mwaka unaofuata.

Hata hivyo, alisema lengo la ofisi hiyo ni kuwa Taasisi ya kisasa kwa kupindi chake cha uongozi.

## Baraza la Wazee laomba kutengewa bajeti

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

BARAZA Kuu la Wazee Mkoa wa Dodoma, wameomba halmashauri, majiji na manispaa, kutenga bajeti za kuwawezesha kutekeleza kazi zao waondokane na hali ya utegemezi.

Mwenyekiti wa Baraza hilo Mkoa wa Dodoma, Mchungaji Peter Mpolo, alisema hayo mbele ya Mkuu wa Wilaya ya Kondoa, Khamis Mkananchi, baada ya kuchaguliwa na kuzinduliwa baraza hilo.

Mpolo, alisema majiji, manispaa na halmashauri, wakiwawezesha bajeti hizo zitawafanikisha kushiriki vikao mbalimbali vitakavyowasaidia kufahamu wajibu wao.

Alisema kuwa wazee wengi kuanzia ngazi ya kijiji, kata, wilaya hadi mkoa hawajui mipaka ya kazi na wanahitaji kuwekewa bajeti hiyo ili wafanye kazi zao kwa ufanisi.

"Tusipojua wajibu na mipaka yetu tunaweza kuingia ambako siyo kwetu kwa maana hiyo tunahitaji kuwezeshwa," alisema.

Pia, Baraza hilo limewaomba Wakurugenzi wa majiji, halmashauri na manispaa kuwaandikia barua watendaji wa kata ili waingie kwenye vikao vitakavyowawezesha kupeleka mahitaji yao.

Mkuu wa Wilaya ya Kondoa, Khamisi Mkanachi, akizungumza kwenye uchaguzi huo na wazee hao wa baraza kuu alisema kuwa serikali imejipanga kuhakikisha inawahudumia katika maeneo mbalimbali ikiwamo afya, lishe na huduma zingine za msingi.

Hata hivyo, Mkanachi, aliwataka viongozi wa Baraza la Wazee waliochaguliwa kusimamia ustawi kwa wenzao kwenye maeneo yote bila kubaguana.

"Mmechaguliwa kwenye nafasi hii ambayo naamini itakuwa ya miaka mitatu, ninawaomba mkasimamie na kutetea haki za wazee ili waweze kupata haki za msingi," alisema.

# Mikakati kudhibiti utumiaji fedha nyingi kuagiza mafuta

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WAZIRI wa Kilimo Prof. Adolf Mkenda amesema serikali imeweka mikakati madhubuti itakayosaidia taifa kuondokana na kutumia kiasi kikubwa cha fedha kuagiza mafuta ya kula kutoka nje ya nchi.

Alisema kuwa hivi sasa Tanzania inatumia kila mwaka kiasi cha zaidi ya Sh. bilioni 500 kuagiza mafuta ya kula kutoka nje ya nchi.

Prof. Mkenda alibainisha hayo jana jijini Dodoma wakati alipokuwa akifungua kongamano la pili la kitaifa la Jukwaa la wazalishaji vijijini (JUWAVITA).

Alisema kutokana na utafiti uliofanywa na wizara yake uhaba wa mafuta ya kula nchini unatokana na viwanda vingi kuzalisha chini ya kiwango.

Alisema hali hiyo inatatokana na uhaba wa malighafi kwa ajili ya kukamua mafuta ya kula hasa mbegu za alizeti.

"Viwanda vingi sana changamoto yake ni mbegu kwa ajili ya kukamua mafuta hivyo vinazalisha chini ya asilimia 100, hali inayosababisha sisi kutumia kiasi kikubwa cha fedha kuagiza mafuta nje," alisema Prof. Mkenda.

Pia, kutokana na hali serikali imeamua kuwekeza katika upatikanaji wa mbegu bora ambazo zitatumika kwa ajili ya ukamuaji wa mafuta.

"Hivi sasa tumepanga kununua mbegu bora za chotara kwa wingi na kuzisambaza kwa wenye viwanda vya mafuta ya kula nchini na wao kuingia mkataba na wakulima ambao watalima kwa ajili ya malighafi za viwanda vyao," alisema.

Kadhalika, hivi sasa serikali imepunguza kero nyingi zilizokuwapo katika uzalishaji wa bidhaa mbalimbali na itaendelea kuweka mazingira rafiki kwa wakulima na wafugaji.

Serikali pia imeamua kuwekeza nguvu katika shughuli za ugani kwa kuongeza bajeti ili kusaidia kada hiyo kutimiza wajibu wake na kuleta tija ambayo ilikosekana kwa muda mrefu.

Mkurugenzi Mtendaji wa ANSAF, waandaji wa Kongamano hilo, Audax Rukonge, alisema malengo ni kuangalia mambo ya kisera katika shughuli za ugani, masoko, uchakataji wa mazao, uvuvi, ufugaji pamoja na kutoa maadhimio ambayo yatalisadia taifa kupiga hatua katika shughuli hizo.





# Rais Mwinyi na ndoto ya ZIPA kuwa kituo kimoja cha huduma

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi, amesema ndoto yake ni kuona kwamba Mamlaka ya Kukuza Uwekezaji Zanzibar (ZIPA), inakuwa na Kituo Kimoja cha Kutoa Huduma.

Alisema hatua hiyo ya kuwa na kituo hicho itasaidia kuondoa urasimu na ucheweleshaji wa kutoa huduma kwa wawekezaji na kuifanya sekta ya uwekezaji kuwa rahisi hapa nchini.

Rais Dk. Mwinyi, aliyasema hayo wakati akizungumza na uongozi wa ZIPA chini ya Mkurugenzi Mtendaji, Shariff Ali Shariff, pamoja na uongozi wa Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC), chini ya Mkurugenzi Mtendaji, Dk. Maduhu Isaac Kazi, mazungumzo yaliyofanyika Ikulu, Zanzibar.

Alisema jambo wanalolifanya na kuendeleza utaratibu wa kukuza ushirikiano ni la busara na lina tija kubwa katika masuala ya uwekezaji nchini na fursa zilizopo zinafaa kufanywa kwa pamoja.

Alisema uamuzi huo wa kuwa na ushirikiano anauunga mkono na kuzitakia maendeleo makubwa taasisi hizo kwa azma ya kufikia lengo lililokusudiwa.

Rais Dk. Mwinyi alisema kuwa ipo haja ya kuimarishwa zaidi utaratibu wa hati ya maelewano (MOU), iliyokuwapo awali na wakati umefika kwa yale yaliyokuwa hayamo yaweze kuingizwa kwenye MOU kwa lengo la kupata tija zaidi kwa pande zote mbili.

Alisema suala la kubadilishana uzoefu kati ya taasisi mbili hizo ni jambo muhimu, hatua ambayo itasaidia kupatikana kwa mafunzo kwa watendaji wa Taasisi hizo kwa azma ya kuimarisha sekta ya uwekezaji nchini.

Dk. Mwinyi amezishajihisha taasisi hizo na kuzitaka kuwa kioo na kielelezo thabiti katika kuhakikisha suala zima la uwekezaji linaleta manufaa kwa taifa.

Naye Mkurugenzi Mtendaji wa ZIPA, Shariff, alisema kwamba ushirikiano unaoimarishwa kati ya taasisi mbili hizo ni njia moja wapo ya kuimarisha Muungano uliopo hasa ikizingatiwa kwamba taasisi hizo zinategemeana.

Alisema ushirikiano huo utasaidia kuendeleza sekta ya uwekezaji nchini na kueleza kwamba ziara ya taasisi ya TIC, Zanzibar ina azma ya kuangalia maeneo ya kushirikiana kwa lengo la kuitangaza Zanzibar.

Alisema kabla ya taasisi kufanya ziara yake hiyo imeanza kazi ya kuitangaza Zanzibar nchini Misri na kuwavutia wawekezaji kuja kuwekeza kiwanda cha dawa.

Pia, alisema hatua zinazochukuliwa kwa pamoja ni kutengeneza hati ya makubaliano, kati ya taasisi hizo na tayari wameshachagua timu ya kufanya kazi wakiwamo wataalamu wa masuala hayo ya uwekezaji.

Mkurugenzi Shariff alimuhahidi na kumhakikishia Rais Dk. Mwinyi kwamba ZIPA inajitahidi kuleta mabadiliko na hivi sasa inatoa vibali vya kazi kwa muda wa dakika 15 iwapo taratibu zote stahiki zimeshafanyika.

Kwa upande wake Mkurugenzi Mtendaji wa TIC, Dk. Maduhu Issac Kazi, alisema taasisi hizo zimedhamiria kushirikiana katika uwekezaji hasa maeneo mbalimbali ikiwa ni pamoja na kubadilishana uzoefu, kushirikiana kwenye suala la huduma kwa uwekezaji na mambo mingine.



Baadhi ya watalii kutoka nchini Ujerumani, wakiangalia zao la Vanila, walipotembelea shamba la Spice Kizimbani, nje ya Mji wa Zanzibar jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Serikali yatambua mchango vyama vya ushirika

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji, Mudrik Ramadhani Soraga, amesema serikali inatambua mchango mkubwa wa vyama vya ushirika katika kuinua hali za maisha ya wananchi wake.

Akizungumza na wanaushirika na wajasiriamali, Kikwajuni, wakati akifungua maonyesho ya bidhaa ikiwa ni maadhimisho ya siku ya ushirika duniani, alisema Serikali imeandaa mikakati imara ya kuimarisha vyama vya ushirika.

Alisema kwa kuthamini michango hiyo, mipango ya mafunzo imeandaliwa na inatekelezwa kwa viongozi, wanachama na watendaji wa vyama vya ushirika kwa lengo la kuvifanyia mageuzi vyama hivyo na kuwa taasisi imara za kiuchumi na zenye uwezo wa kuzalisha bidhaa zenye ubora na viwango ili kupata nguvu za ushindani katika soko.

Pia, alisema serikali itachukua juhudi za kutatua changamoto ya masoko kwa bidhaa zinazozalishwa na wanaushirika na wajasiriamali kuinua uwezo wa kupatana bei katika soko na kusaidia kuimarisha miundombinu, vyumba vya kuhifadhia mazao pamoja na barabara za ndani.

Hata hivyo, alisema serikali imeanzisha wizara maalum ya uchumi wa bluu na kuwaunga mkono wanaushirika kwa kuwawezesha ili kutumia fursa zilizopo katika sekta ya uchumi wa bluu, kutoa utaalamu wa kisasa ukiongeza thamani bidhaa zao ikiwamo chumvi, mwani na viwanda vya usarifu ili kuzalisha na kujipatia ajira na kipato endelevu.

Naye Mwenyekiti wa Faraja Union Limited, Suleiman Ame Vuai, alisema wajasiriamali ni chachu kubwa katika kukuza uchumi wa viwanda na kuchangia Pato la Taifa.

Alisema kuna kila sababu ya kuwaunga mkono katika biashara zao ili kutimiza malengo yao waliyojikusudia katika kujipatia riziki za kuendeleza maisha wao na familia zao.

Kwa upande wake mtaalamu wa masuala ya mabadiliko ya hali ya hewa, Saadat Said Mohd, akielezea kuhusu zao la mwani aliiomba serikali iwapatie viwanda ili wapate kusarifu vyema bidhaa zao ikiwamo losheni, sabuni na bidhaa zingine.

# Wanafunzi wapewa mwongozo masomo yenye tija

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Elimu Mohammed Said, amewataka wanafunzi kusoma masomo yenye tija kwa serikali ili kupata wataalamu wa kada mbalimbali nchini ikiwamo fani ya ardhi.

Kauli hiyo aliitoa wakati akifungua maonesho ya pili ya elimu ya juu Zanzibar yaliyoziishirikisha taasisi mbalimbali za elimu na vyuo vikuu vya Zanzibar na Tanzania Bara yaliyofanyika katika Uwanja wa Mapinduzi Square Mnarani, Mjini Unguja.

Alisema Zanzibar ina uhaba mkubwa wa watalaamu wa fani hizo kama vile wa mipango miji, wapimaji ardhi, wachoraji ramani na watalaamu wingine wanaotokana na fani hiyo.

Alisema kuwa maonesho hayo yanalenga kujua miongozo na taratibu ya kujiunga na vyuo vya elimu ya juu na kupata fursa za kujua nafasi za masomo zinazotolewa nchini na nchi jirani.

Pia, aliahidi kukiongezea nguvu kitengo cha elimu ya juu ili wanafunzi wapate taaluma na kufaidika katika siku za baadaye.

"Kwa wito huu ninaokupeni haina maana kwamba nyote mkajaze fomu katika masomo haya, bali ni kujijenga katika fani mbalimbali ikiwamo Uhasibu, Mawakili, Wanasheria na nyingine, lengo letu ni kuona tunapata wataalamu katika maeneo yote kila mwaka kwani tunahitaji watalaamu ikiwamo kwenye sekta ya usafiri, anga, afya, maji na maeneo mingine," alisema.

Aliwataka wanafunzi hao kwenda katika taaluma zote ambazo serikali inazihitaji kupata watalaamu wa ndani ya nchi ili kwenda sambamba na mpango mkuu wa nchi na matarajio kwa sekta binafsi.

"Tunasikia uchungu kuona mwanafunzi amemaliza masomo, lakini anapiga hodi kuhangaika kila eneo kutafuta ajira, lakini kila anapokwenda nafasi zimeshajazwa," alisema.

Naye Mwenyekiti wa Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania, Professa Mayunga Nkunya, ameipongeza Wizara ya Elimu kwa kuyaendeleza maonesho hayo ambayo ni muhimu kwa wanafunzi katika kujiwekea malengo yao ya baadaye. Alisema maonesho hayo kwa Tanzania yameanza miaka 10 iliyopita na wameona manufaa yake hasa kwa wanafunzi kujua mambo mbalimbali katika kujiunga na vyuo vikuu na kupanua fursa za maisha.

Alisema Tume ya Vyuo Vikuu (TCU), inafanya mambo makuu matatu muhimu ikiwamo kuhakiki ubora wa elimu ya juu nchini Tanzania, kutoa ushauri wa vyuo vikuu serikalini kwa wanafunzi na jamii nzima ya Tanzania, kutoa msaada wa vyuo katika uendeshaji wa vyuo hivyo na elimu ya juu na ukuaji wa vyuo hivyo Tanzania.

Alisema maonesho hayo yaliyoandaliwa na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kupitia Wizara ya Elimu, TCU yanawasaidia katika jukumu la kutoa ushauri na msaada kwenye vyuo vikuu na kwamba ni fursa kwa wanafunzi kuona na kuifahamu elimu ya juu nchini.



**WEEKND, ANGELINA JOLIE KUNANI?** Uk.14

Nipashe MWANGA WA JAMII

BT BURUDANI TELE

JUMAMOSI JULAI 3, 2021



## HAIKUWA RIZIKI

# Sababu Diamond kushindwa BET hizi hapa

USIKU wa Julai 28, mwaka huu, mwanamuziki nyota kutoka Tanzania, Diamond Platnumz, ameshuhudia ndoto yake ya kupata tuzo ya BET ikiyeyuka ghafla na badala yake ilinyakuliwa na msanii kutoka Nigeria, Burna Boy .

Ushiriki wa Diamond katika tuzo hizo kwa mwaka huu, ulikuwa faraja kwa mashabiki wa muziki wa Afrika Mashariki, kutokana na ukubwa wake na heshima waliyopata wananchi wa ukanda huo.

Hata hivyo, kuikosa tuzo hiyo imeelezwa inatokana na sababu nyingi, lakini kulingana na wachambuzi wamezitaja kuwa ni utambulisho wa muziki, utandawazi na ukosefu wa mbinu za ushindi.

Wakizungumza na BT, wachambuzi hao wamesema tuzo hiyo yenye hshima imekwenda Nigeria, kutokana na wasanii wao kuwa na akili nyingi kutafuta maisha na kutunza utambulisho wa muziki.

Wamesema isingekuwa rahisi Diamond, kurudi na tuzo hiyo, wani Wanigeria walitumia mbinu mbalimbali kuomba kura pamoja na kuwatumia raia wa nchi hiyo ambao wanaishi ughaibuni.

"Wenzetu wamewatumia kwa kiasi kikubwa raia wao wanaoishi Ulaya na Marekani kupata kura, sisi hatuna watu wengi na ndio maana tukakwama," amesema mmoja wa wachambuzi hao.

Waeeleza sababu nyingine ni matumizi ya majaji zaidi ya 300, wanaochagua mshindi kutoifahamu vizuri Tanzania kuliko Nigeria.

Wamesema muziki wa Nigeria unapigwa na kuuzwa Marekani, tofauti na Bongo Fleva, ambao unatamba Afrika Masharki pekee.

Aidha, wametaja jambo lingine lililochangia tuzo hiyo kutokuja nchini, ni muziki wa Bongo Fleva kutokuwa na utambulisho rasmi kama ilivyokuwa Afrika Magharibi na Afrika Kusini.

"Hatuna utambulisho wa muziki wetu, leo hii tunaiga muziki wa Afrika Kusini, tunatumia ujanja tu tofauti na wenzetu ambao wanaulinda muziki wao," amesema.

BASI SAWA

## Calisah amtibua tena Jux



MWANAMITINDO Calisah, amemkabili mwanamuziki wa R&B, Jux, kwamba ana miaka mingi katika tasnia ya muziki lakini hakuna alichokifanya nje ya nchi.

Amesema shoo zake kubwa ni za ndani ya nchi, hivyo inampa tabu kujua kwa nini hajatoka hata kwenda Nigeria kufanya onyesho.

Sijui kwa nini hajatoka nje licha ya kukaa katika gemu kwa miaka 10, sijui hana pesa au ameamua tu, anaachwa nyuma hata wasanii kama Harmonize," amesema Calisah.

## Majani aiacha rasmi Bongo Fleva alioanzisha



MTAYARISHAJI mkongwe wa muziki wa kizazi kipya nchini, P-Funk Majani, ametangaza kung'atuka rasmi katika kazi hiyo baada ya kuitumikia kwa miaka 28.

Wiki hii, Majani ambaye ameamua kuanza maisha ya kuandaa filamu na video za muziki, amesema muda huo wa kuibua muziki umemtosha na sasa anatafuta nafasi nyingine.

"Nimeishi studio kwa zaidi ya miaka 28, miaka yote ya kusikiliza kelele za vyombo vya muziki usiku na mchana, miaka 28 ya kuandaa nyimbo za watu tofauti waliofanya vizuri katika nyakati tofauti. Maisha na umri vimenitambulisha kwenye ulimwengu mwingine, ni muda ambao nahitaji zaidi utulivu, kufurahia, kusafiri sehemu tofauti nikiwa na kamera,"amesema Majani katika ujumbe wake aliouweka kwenye ukurasa wake wa Instagram.




# Lady Du kuwachezesha 'Amapiano' Dar

MWANAMUZIKI na DJ kutoka Afrika Kusini, Lady DU, anatarajia kuwachezesha mashabiki wake wa Dar es Salaam, mtindo mpya wa muziki maarufu kama Amapiano.

Lady DU amejipatia umaarufu kupitia muziki huo anatarajia kutua nchini Julai 2, mwaka huu kwa ajili ya kufanya shoo yake Masaki.

Staa huyo ametoa nyimbo zinazotikisa kama Soft Life, Dakiwe, Catalia, Possible na Woza.




# Saraphina awachambua washindi BSS

MSANII wa muziki wa Bongo Fleva, Saraphina Michael, ametoboa siri kwa nini baadhi ya washiriki wa Bongo Star Search (BSS), wanashindwa kuendelea mara baada ya kushinda.

Akizungumza katika Kipindi cha Supa Breakfast cha East Africa Radio, mwanamuziki huyo anayetamba na wimbo wake wa "Singo" amesema baadhi wanalewa na ushindi na kuona wamefika .

"Wengi wakienda kushindana BSS wanafikiri akishashinda ndo basi, ila uhalisia ni kwamba baada ya kushinda kazi inaanza tena inabidi upambane kama uko underground na inasaidia kukupa platform kama mimi," amesema Saraphina.

# Enzi hizoo ziliwachengua

**Na Adam Fungamwango**

WENYE miaka ya 1980, hadi katikati ya miaka ya 1990, kabla ya televisheni kuenea majumbani, vijana na watoto wengi walikuwa wakienda maeneo mbalimbali ili kuona sinema.

Wengine walienda kwenye majumba makubwa ya sinema. Hao ni kwa wale kwenye uwezo. Wengine walikwenda maeneo ambao yalikuwa yana afadhali kidogo. Lakini wengi wao hasa watoto walikuwa wakienda kwenye sehemu ambazo kwa sasa zinaitwa 'vibanda umiza'.

Huko utakuta mtu kazungushia tu magunia na ndani kaweka televisheni yake, akionyesha filamu mbalimbali.

Achilia mbali filamu za Kichina, ambazo nyingi ni za sanaa za mapigano, na kihindi ambazo tutakuja kuzizungumzia siku nyingine.

Kulikuwa na filamu nyingi maarufu za kizungu ambazo hakuna kijana au mtoto ambaye alitaka kuzikosa. Leo tunakwenda kuangalia filamu hizo.

**WAR BUS**

Ni filamu marufu sana kwa Wabongo, ambayo ilitoka mwaka 1985. Mastaa wa picha hii ni Daniel Stephen, Romano Kristoff na Urs Althaus.

Msingi wa picha hii ni vita ya Vietnam. Ni makomandoo watatu wa Kimarekani waliokwenda kuwaokoa mateka walioshikiliwa na 'wavete', kama walivyokuwa wakiitwa watoto wakati huo.

Kilichovutia zaidi watazamaji wengi wa filamu hiyo, siyo operesheni hiyo, bali ni staili ya makomandoo hao ambao waliamua kuteka basi ya shule na kulitumia kama usafiri wa kwenda kuwaokolea watu wao. Ile staili ya ulinzi wa mmoja kukaa mbele ya boneti la basi, mwingine juu kwa ajili ya ulinzi, mwingine ndani, pamoja na mbwembwe zao, ndiyo msingi wa picha hii kupendwa.

**AMERICAN NINJA**

Hii pia ni filamu ambayo iliwanyima watu usingizi, ikitoa mwaka 1985 kama 'War Bus'.

Wakubwa, vijana na watoto wa Kibongo waliipenda sana filamu hii, ikimhusisha staa mmoja anaitwa Michael Dudikoff. Huyu ni askari wa Kimarekani ambaye pia ana ujuzi mwingine wa kupigana na watu wanaitwa maninja, ujuzi alioupata akiwa mdogo.

Humu anatwangana na maninja kisawasawa na kushinda, kiasi cha kuwa moja ya filamu bora sana na kukumbukwa hadi leo.

**NO REAREAT, NO SURRENDER**

Filamu hii ilitoka mwaka 1986. Hii siyo ya kivita kama 'War Bus'. Wala siyo ya mapanga na sanaa za kininja. Picha hili ni la sanaa wa mapigano. Humo ndani zimepigwa balaa.

Stelingi kwenye filamu huu ni staa aliyekuwa maarufu sana wakati huo, Jean Claude van Damme. Huyu alisifika sana kwa mateke ambayo ndiyo yaliyokuwa yanampa zaidi ushindi. Ni moja kati ya filamu maarufu na iliyopendwa sana.

**KOMANDO KIPENSI**

Jina halisi ya picha hili ni 'Deadly Pray'. Lakini nadhani hadi leo si wengi wanaojua jina halisi ya filamu hii. Lakini ukiwaambia 'Komando kipensi', kila mtu atasema anaifahamu.

Sidhani kama kuna mtoto au kijana wa miaka ya 1980 mpaka 2000, ambaye haifahamu filamu hii. Ilitoka mwaka 1987.

Jamaa anaitwa Troy Donahue, au kwa jina la picha ni Mike Danton. Huyu ni jeshi la mtu mmoja. Anapigana akiwa amevaa pensi tu, ndiyo maana wakamwita hivyo. Alimchokoza wenyewe. Walikuwa hawajui kuwa ni mwanajeshi mstaafu. Walitaka kumfanya chambo. Ikawa ni vita vya ajabu.

**DELTA FORCE**

Ilitoka mwaka 1986. Ni moja kati ya filamu maarufu sana kwa Wabongo wakati huo. Staa wa filamu hii ni mkongwe Chuck Norris. Ni picha la kivita.






# Penye penzi hapakosi tezi

**Na Adam Fungamwango**

MSONDO Ngoma waliwahi kuimba wimbo mmoja uitwao 'penye penzi hapakosi tezi.' Wakiwa na maana kuwa siku zote kwenye mapenzi, hapakosi watu ambao watayatoa kasoro na kutaka kufanya figisu zozote zile ili wapendanao wafarakane na kuachana. Lakini kama wote, au mmoja atakuwa anababaishwa na kelele, basi penzi linaota tezi.

Leo tunaiangalia filamu iitwayo 'Rossa'. Imechezwa na wasanii Said Lukamba, Vanesa Widambe, Mzee Makwati, Upendo Jaspa, Jenifa Salum, Mwanaidi Dihomi na wengineo.

Ni filamu inayoonyesha mtawala wa himaya moja ya Chiwale, ambaye ni mwanamke anayehangaika kupiganía penzi la binti yale Dora.

Ni kwamba binti yake alimpenda kijana mmoja aitwaye Lwigila. Binti mfalme akafa akaoza, lakini kijana huyo penzi lake lilikuwa kwa binti mwingie Rossa. Huyu ni binti wa kawaida tu kwenye himaya hiyo. Mtawala aliitisha mkutano wa vijana wote nyumbani kwake ili binti yake Dora achague mchumba. Walikuja na Dora alipita kwenye mstari kuchagua, lakini Lwigila hakuwepo. Huyo ndiye alitaka kumchagua. Hali ikawa mbaya. Walipoondoka Dora alimlilia mama yake, Mtawala akaanza kutumia nguvu kutaka kulazimisha.

Kwanza akaenda nyumbani kwa kina Lwigila na kupiga mkwara wa nguvu. Akaenda nyumbani kwa msichana Rossa na kudai uchumba wa Lwigila na Rossa yeye kama mtawala hautambui.

Baada ya kutumia mkwara wa utawala wake kushindwa, sasa ilibidi mtawala atumie ndumba. Rossa akafanywa ndodocha na Lwigila akawa mwendawazimu. Msukule wa Rossa ukatoka ulikowekwa na kukimbilia kusikojulikana. Huko ulikutana na kijana mmoja ambaye aliuchukua na kuupeleka kwa mganga, ukapona. Akarudi Rossa yule yule.

Huku nako Lwigila aliponyeshwa na masharti ya kumuoa binti wa mtawala ili awe mfalme.

Wakati wakiwa kwenye sherehe ya Lwigila na binti mtawala, ghafla anamuona Rossa akiwa ameongozana na kijana mmoja. Wote walionana. Kila mmoja kwenye hadhara alimuacha aliyekuwa naye na kukimbiliana. Wakakumbatiana.



# Weeknd, Jolie kunani?

MWANAMUZIKI wa Canada, Weeknd na mcheza filamu maarufu, Angelina Jolie, imeelezwa wameingia katika dimbwi la mapenzi mazito.

Inadaiwa wawili hao wamekutwa siku ya Jumanne ya wiki hii, wakila bata katika hoteli moja ya kifahari ya Giorgio Baldi iliyopo Los Angeles.

Chanzo cha karibu kimeeleza baada ya kula pamoja chakula cha kitaliano, wawili hao walienda katika mgahawa mmoja kila mtu kivyake ili kuhofia kuvuja kwa uhusiano wao.



## Maskini Chameleone anajiondokea

MASHABIKI wa mwanamuziki wa Uganda, Chameleone, pengine wana muda mchache kumuona jukwaani baada ya yeye mwenyewe kutangaza anafikia ukingoni.

Chameleone ambaye ametamba na nyimbo zake 'Katupakase na Jamila; amesema akifikisha umri wa miaka 50, anaacha muziki.

"Nina miaka 42, nimebakiwa miaka minane nistaafu muziki, nazidi kurudi nyuma siwezi tena kuruka jukwaani katika maisha yangu yajayo, amesema.

## Bill Cosby afurahia maisha uraiani

MSANII wa uchekeshaji, Bill Cosby, ameanza kufurahia maisha ya uraiani baada ya kukaa ndani akitumikia adhabu ya miaka 10 kifungoni.

Muigizaji huyo amekaa miaka mitatu kufuatia kupatikana na hatia ya kumnyanyasa kingono na kutumia dawa za kulevya dhidi ya mwanamke mmoja aliyeitwa Andrea Constand mwaka 2004.

Hata hivyo, Mahakama kuu Pennsylvania, ilibatilisha hukumu yake baada ya kufanya mapitio ya hukumu na kuona haki zake zilikiukwa wakati wa kusikilizwa kwa kesi yake.






## Wizkid umeyataka mwenyewe

NYOTA wa muziki kutoka Nigeria, Wizkid, anatuhumiwa kumlipa mwimbaji wa Marekani, Rihanna ili autangaze wimbo wake mpya "Essence" katika mtandao wa kijamii.

Katika akauti ya Istagram, Rihanna alionekana mubashara akiucheza wimbo huo.

Hata hivyo, mashabiki wake wameonekana kukasirishwa na kumtuhumu Wizkid, kuwa alitoa pesa ili Rihanna, aweze kuutangaza.

## Mzee Edochie ulijuaje wanavaa vigodoro?

MWIGIZAJI mkongwe wa Nigeria, Peter Edochie, ameelezea wasiwasi wake kutokana na wanawake wengi nchini humo kufanya upasuaji wa kurekebisha maumbile yao.

Akizungumza kupitia kituo kimoja cha Runinga, Edochie, amesema kwa sasa imekuwa vigumu kumpata mwanamke mwenye umbo la asili ambaye anafaa kuolewa.

"Leo ni vugumu kumtafuta mwanamke ambaye yupo kama alivyoumbwa,wanavaa nywele bandia, ni vigumu kumpata mwanamke wenye vichunusi au mwenye makalio yaliyoumbwa na Mungu," amesema.



ALIYOANZA NAYO MAMA...

# Ukaguzi ulivyofukua mlolongo wa mashimo ya TEHAMA serikalini

## ●Kasoro zilizoanikwa 2016 zimebaki vilevile

**Na Sanula Athanas**

MNAMO Machi 28 mwaka huu, akiwa na siku tisa pekee tangu kuapishwa kushika wadhifa wa sasa, moja ya hatua zake muhimu za awali, Rais Samia Suluhu Hassan, alipokea Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kwa mwaka 2019/20.

Ndani ya mlolongo mrefu wa wasilisho lake, CAG, Charles Kichere, alichambua kasoro nyingi zilizoko katika ya mifumo ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) na utendaji wake serikalini.

Kimsingi, mchakato wa kuwa na sera ya TEHAMA serikalini ulianza rasmi mwaka 2003, ikiwa ni kuendana na mageuzi yanayochukua kasi duniani katika eneo hilo.

Baada ya sera hiyo kudumu kwa zaidi ya muongo mmoja, mnamo Mei 16, 2016, serikali ilizindua sera hiyo iliyofanyiwa mapitio, na miezi mitano baadaye, Novemba 2016, ukiwa ni mwanzo wa serikali ya awamu ya tano, mwongozo maalum wa matumizi yake ukazinduliwa.

Kwa mujibu wa Tovuti Kuu ya Serikali, miongoni mwa maudhui muhimu yaliyoshuhudiwa katika zama hizo za uzinduzi miaka mitano iliyopita, yalijumuisha mtazamo wa kuelekea kwenye manufaa katika kipindi hicho cha uzinduzi yakiwa na ufafanuzi:

Mosi ni manufaa ya mtandao unaoihakikishia serikali inakuwa kama taasisi moja kwa kuunganishwa na TEHAMA huku usalama na faragha za taarifa za serikali na watumiaji zikiimarishwa.

Pili kuwapo lengo kuu lenye mtazamo wa kurahisisha utendaji kazi wa serikali na kuboresha kwa kiasi kikubwa utoaji wa huduma kwa wananchi.

Tatu ilibeba mtazamo mahsusi wa kupunguza gharama kubwa ya kuwapo mifumo ya TEHAMA serikalini, matumizi shirikishi na inayotumika kirahisi kwa walengwa wa huduma husika.

Pamoja na kuwapo sura hiyo ya manufaa wakati wa kuzindua mwongozo, tayari kulikuwa na angalizo la kasoro inayopaswa kurekebishwa inayonukuliwa kwa ujumbe ufuatao utokanao na angalizo la uzoefu wa matumizi ya TEHAMA serikalini kwamba:

"Kuna uwezekano kuwapo utengenezaji au ununuzi wa mifumo ya TEHAMA isiyozingatia mahitaji halisi ya taasisi na serikali kwa jumla na uwapo wa mifumo inayoweza kuhatarisha usalama wa taarifa za serikali.

"Changamoto hizo na nyingine kadha wa kadha ndizo zilizosababisha serikali kuweka miongozo na viwango thabiti katika TEHAMA itakayowezesha taasisi za serikali kuzikabili."



Mwakilishi wa Msajili wa Asasi za Kiraia, Charles Mpaka, akikata utepe kuzindua Ripoti za Uwajibikaji mwaka huu zinazochambua maudhui ya TEHAMA serikalini. Anayeshuhudia, wa kwanza upande wa pili ni Ludovick Utouh, CAG mstaafu. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

Ushauri wa kiserikali uliotolewa kuweka sawa dosari hizo ulitaka kujengwa uelewa wa viwango stahiki vya TEHAMA vinavyohitajika serikalini kwa sekta binafsi na umma.

### JICHO LA CAG

Mbali na CAG kukiri kasi ya kutumika TEHAMA serikalini, bado ana angalizo maalum kupitia ripoti ya ukaguzi wake ya mwaka huu akiwa na orodha ya udhaifu katika maeneo ya utekelezaji.

CAG Kichere, anasema bado kuna ukiukwaji wa maagizo ya Sera ya Taifa ya TEHAMA ya Mwaka 2016 inayozitaka taasisi zote za umma nchini kuandaa sera na mpango mkakati wake wa TEHAMA utakaoziongoza, huku akitoa mifano ya ushahidi katika taasisi na ofisi za kiserikali 18.

"Pia, sera na mipango mikakati iliyopo haiendani na kanuni za fedha katika taasisi zilizokaguliwa," CAG anaongeza huku akiwa na orodha ya upungufu kadhaa.

CAG anasema Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma (PPRA) ambayo ina haki na mamlaka katika kusimamia ununuzi kitaifa, haikuwezeshwa kuzifikia kanzidata na seva za mifumo hiyo ya TEHAMA inayotumika serikalini iliyonunuliwa nje ya nchi.

Kwa kuzingatia tafsiri hiyo, PPRA ambayo inaongozwa na kanuni ya kitaaluma ya ununuzi kwamba mfumo wa ununuzi nchini ni sharti usimamie miongozo mitano, maarufu '5Rs', kwa maana ya bidhaa au huduma kununuliwa ikiwa na usahihi kwenye: bei, muda, viwango, idadi na chanzo, haijafanikisha mwongozo wake hasa kwenye chanzo.

"Vilevile, mfumo wa TANePS (ilikonunuliwa huduma) haujaunganishwa na mifumo mingine ya kiserikali, mfano: Mfumo wa Bajeti ya Serikali Kuu na Mfumo wa Malipo ya Serikali (GePG)," CAG anataja na kufafanua kilichodokezwa kwenye angalizo la mwaka 2016:

"Kutounganishwa kwa mifumo hii ni kinyume cha dhana ya kuwa na mifumo ya TEHAMA ambayo inarahisisha kazi na badala yake kufanya kazi kuwa ngumu na zenye mlolongo mrefu kiutendaji."

Mdhibiti huyo wa hesabu za serikali pia analaumu udhaifu aliogundua kwa Mfumo wa TEHAMA wa Bajeti ya Serikali (CBMS) kwamba hauna uwezo wa kuzuia matumizi ya zaidi ya kiwango kilichoidhinishwa.

Katika eneo la ukusanyaji wa mapato ya serikali, CAG aligundua mfumo wa TEHAMA uliopo ulikuwa na ualakini unaoshindwa kutekeleza zaidi ya mambo muhimu matano ambayo ni sehemu ya kanuni, sheria na maelekezo ya kiserikali.

Hapo kuna suala la kushindwa kukokotoa ushuru wa huduma, ada za ujenzi wa majengo na adhabu; kutoonesha kiasi sahihi cha fedha zisizowasilishwa benki; kukosekana uwiano wa muda wa leseni za biashara unaooneshwa katika mfumo dhidi ya zilizopo katika kanuni za biashara.

Anaitaja kasoro nyingine ni kwa mfumo huo wa TEHAMA kushindwa kutunza kumbukumbu za miamala ya makusanyo katika Mashine za Kukusanya Mapato (POS) ambazo ama zimepotea au kuharibika; na uwezekako wa kuvurugwa taarifa za mashine kutokana na sababu za udhaifu wa udhibiti wake kielektroniki.

Eneo lingine la dosari kwa mujibu wa CAG Kichere ni kuwapo mifumo inayofanya kazi zinazofanana, hali ambayo anaitafsiri ni dalili ya kutokuwapo mawasiliano sahihi ya kiutendaji kati ya wizara, idara na taasisi za kiserikali.

### KWA NINI UPUNGUFU HUO?

CAG anaelekeza mbali jicho lake kitaaluma, akianza na kukosoa eneo la maudhui ya kilichozinduliwa mwaka 2016 kuhusu Sera ya TEHAMA serikalini, hasa katika mipango mikakati, akiitaja hadi sasa haiendani na mahitaji na teknolojia hiyo, hivyo kuua ubora wa kazi za kielektroniki katika kufanikisha lengo kuu la kupatikana ufanisi katika utendaji.

Pia anataja kuwapo kasoro hizo kunafungua mianya kwa watumishi wasio waadilifu kutekeleza uhalifu dhidi ya maslahi ya umma, akitoa mfano wa kilichojiri kutoka Idara ya Uhasibu kwenye halmashauri mojawapo ya mkoani Ruvuma ambako serikali ilipoteza zaidi ya Sh. milioni 270.

CAG Kichere anasema TEHAMA duni imeipotezea bajeti wajibu na haki yake kuwa nyenzo ya udhibiti wa shughuli za fedha serikalini, huku akitoa mfano hai wa kuwapo taasisi sita za kiserikali zilizotumia ziada ya jumla ya Sh. bilioni 24.41 nje ya kiwango kilichoidhinishwa katika mwaka wa ukaguzi (2019/20).

Vilevile, ananyoshea kidole athari za kuwapo mifumo miwili au zaidi inayofanya kazi zinazofanana kwamba ni hatua inayoongeza serikali gharama zisizo za lazima katika uendeshaji na matengenezo, huku akiwa na ufafanuzi zaidi kwamba:

"Kukosekana kwa mwingiliano (lack of interlink) baina ya mifumo ya TEHAMA inayotumiwa serikalini kunaongeza mianya ya wizi na ubadhirifu wa fedha za umma."

### NINI KIFANYIKE?

Taasisi ya WAJIBU inazimulika dosari hizo na kuishauri serikali kuzitafutia ufumbuzi kwa kuchukua hatua tano ambazo Meneja wa Utafiti na Miradi wa taasisi hiyo, Moses Kimaro, anazitaja kuwa ni:

"Kuunganisha mifumo inayofanya kazi zinazofanana (PlanRep dhidi ya TiMES, IFT-MIS dhidi ya GARI-ITS na SIS dhidi ya ASC) na kutengeneza moduli ambazo hazipo katika mifumo hiyo.

"Kuunganisha mifumo ambayo haiwasiliani (TANePS na mifumo ya MUSE, PLANREP, CBMS na GPSA); kuongeza udhibiti wa matumizi ya mifumo ya TEHAMA.

"Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) ifanye uchunguzi na kuwafikisha mahakamani watendaji wanaotuhumiwa kwa vitendo vya rushwa, udanganyifu na ubadhirifu katika mifumo ya usimamizi wa makusanyo na matumizi ya fedha za umma.

"Kuhakikisha seva na kanzidata za mifumo (mfano TANePS) zinamilikiwa, zinaendeshwa na zinasimamiwa na taasisi za serikali na siyo watu au taasisi binafsi."

Mkurugenzi Mtendaji wa WAJIBU, Ludovick Utouh, anatahadharisha kuwa umiliki wa seva unapofanywa na watu au taasisi binafsi, unahatarisha usalama wa siri za serikali, hata kuvurugwa taarifa za mapato ya serikali.

Utouh, aliyekuwa CAG kwa miaka minane kuanzia 2006, ana angalizo kwamba: "Kitendo cha kununua mifumo kutoka nje na seva zake kuwa nje ya nchi, ni hatari katika ulinzi wa siri za serikali. Tunajiweka wenyewe kwenye hatari kubwa."

Makamu Mwenyekiti wa Kamati

INAENDELEA UK. 16



SIKU 100 ZA RAIS SAMIA IKULU

# Machinga Mtaa Makoroboi, Mwanza watabasamu Mama kutembelea vijana

## ●Wakumbuka mbio, rumande, kufilisiwa ●Awapa 'tano' ya kila kitu kwenye uchumi

**Na Anthony Gervas, Mwanza.**

VIJANA ni kundi muhimu katika taifa lolote duniani. Nchini, Ripoti ya Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2012 inatamka katika kila watu 12, wanne kati yao ni vijana wa umri kati ya miaka 15 hadi 35.

Ni tafsiri ya kisera na kisheria, ikichanganywa ikiwagusa pia wenye umri unaokadiriwa miaka 45 hadi 50, na si haba wanaangukia ujana.

Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na Watu Wenye Ulemavu ina takwimu za makadirio Tanzania ina vijana milioni 20.7 na ndiyo nguvu kazi kuu ya taifa inayotegemewa, wakiwa ndio wazalishaji mali wakubwa.

Rais Samia Suluhu Hassan, alipozungumza na vijana wa mikoa ya Mwanza, Kagera, Mara, Shinyanga, Geita na Simiyu, aliwaambia wao ndio wenye uthubutu wa kubeba maono na matarajio ya taifa, pia wanaangukia mtihani wa ajira.

**AJIRA VIJANA.**

Rais Samia anasema, hadi sasa serikali yake imeshachukua hatua ngumu, ikiwamo kukabiliana ana uhaba wa ajira akiuifanyia kazi. Analalamika bado hali si nzuri hadi sasa, hasa katika ulingo wa ajira kwa vijana na asilimia 11.4 ya vijana hao wenye uwezo wa kufanya kazi, hawana ajira.

Pia, serikali inataja takwimu ya mfano, katika nafasi 9,600 za ajira ilizotangaza, hadi siku tano kabla ya kufunga pazia za maombi, ilishapokea barua 120,000.

Rais Samia alipokuwa mkoani Mwanza hivi karibuni, wamekuwa vijana wakiomba ajira bila mafanikio, hata kulazimika kujiajiri katika sekta binafsi.

Anakumbusha ajenda kuhusu uhai, usalama na maendeleo iko kwa vijana, Rais Samia anaendelea na ufafanuzi: "Serikali ya Awamu ya Sita nataka isheheni viongozi vijana.

"Wengi watakuwa wale wa miaka 1970 na 1980, ni mfumo tuliouanza na mtangulizi wangu Hayati Dk.John Magufuli miaka mitano iliyopita wakati mimi nikiwa Makamu wa Rais, kwa sababu wanachapa kazi." .



Kijana machinga, Samwel Amos, katika kibanda chake cha viatu, kwenye soko la Makoroboi, jijini Mwanza. **PICHA: ANTHONY GERVAS.**

**MTAA MAKOROBOI**

Hapo ndiko wanakopatikana vijana wengi Machinga wa jijini Mwanza. Kati yao yupo Samwel Amos,

mjasiriamali wa viatu vya kinamama na watoto, aliyedumu nayo tangu mwaka 2009, alipokuwa na umri miaka 19.

Anakumbuka misukosuko aliyoipitia, ikuwamo vipigo vya mgambo wa jijini Mwanza, kuwekwa rumande, bidhaa zao kupokwa, hata wakafilisika mitaji yao.

Kijana Amos anasimulia, kwamba wakati huo serikali ya mtaa haikuwawekea mfumo mzuri wa kibiashara, hata wakaishia kufukuzwa kutoka katikati ya jiji, wengi walipokuwa wanapanga bidhaa zao eneo la Mtaa wa Makoroboi, anakopataja kuna wateja wengi wa Mwanza na nje ya mkoa.

Anakumbuka alivyowakimbia mgambo kujinusuru, huku nyuma bidhaa zake zikikusanywa na kupandishwa kwenye gari la wakamataji hao.

Machinga huyo wa Mwanza, analalamika matukio hayo yaliyomfilisi mtaji hata kumrudisha nyuma akaanza upya kibiashara na ilikuwa hali mbaya zaidi kwa walioko mitaji.

Katika hilo, bado anakiri udhibiti uliowalinda kutoka kwa Hayati Dk.John Magufuli na sasa kuendelezwa, na makamu wake Samia Suluhu Hassan, ambaye sasa ni Rais, una mchango mkubwa wa kuwashushia pumzi.

Amos anasema hadi sasa mtaji wake bado ni mdogo na anaomba taasisi za kifedha zifungue milango ya kuwakopesha kwa riba nafuu.

Pia, anataja kinachomshushia pumzi ni faida kidogo aliyoambulia kibiashara, imemwezesha kununua kiwanja cha makazi cha Sh. milioni 1.2 na ameshaanza kujenga nyumba ya vyumba vitatu, akiwa baba wa watoto watatu.

Mbinu yake kibiashara anataja ni kuuza viatu vya wanawake na watoto, kwa sababu kimasoko wao huvaa viatu muda mfupi na kubadilisha vingine, kulingana na fasheni.

Anapasifu Makoroboi, kuwa eneo linalomfaa kwa mauzo, akitaja kila siku anapata kati ya Sh.50, 000 hadi 100,000, pale biashara 'inapochanganya.'.

**MACHINGA KUKOPESHEKA**

Makamu Mwenyekiti wa Soko la Makoroboi, Abedy Gideon, anasema awali Machinga wa mahali hapo hawakukopesheka, kwa sababu hawakuwa na chombo rasmi cha kuwatetea kibiashara, lakini baada ya kupata chombo, sasa wanakopesheka kutoka taasisi za kifedha.

Gideon anasema, mwanzo hawakuwa na makao maalum na walifanya biashara pasipo eneo la kudumu, ila sasa anaisifu serikali kusikia kilio chao, wanafanya biashara bila ya kero yoyote.

Anakumbuka machungu ya machinga zama zilizopita, akitamka: "Mgambo wa Mipango Miji walikuwa wakitembea na Mwanasheria wa Jiji, polisi na hakimu. Wanapokukamata, wanakupandisha kwenye gari na baadaye kusomewa mashtaka yako, hukumu inatolewa pale pale unapelekwa gerezani Butimba kutumikia kifungo cha miezi sita."

Gideon anakiri binafsi hakuwahi kuhukumiwa kifungo hicho, ila yalimpata mateso ya kuwekwa rumande na kupokwa mali. Sasa anaiomba serikali isaidie kuwajengea uwezo wa kukopa na kukuza biashara zao.

"Makoroboi ni maarufu nchini. Ni kitovu cha biashara mbalimbali, ukifika jiji la Mwanza bila kufika Makoroboi bado hujafika Mwanza," anatamka na kuendelea:

"Biashara zote kubwa na ndogo ziko mtaa huu, wapita njia wengi hupita mtaa huo sababu uko katikati ya jiji hilo, bidhaa za kila aina zipo, ndiyo maana Machinga wengi wamefurika hapo kuliko maeneo mengine."

Analalamika kwamba, licha ya kuuanza 'umachinga' mwaka 2004, hadi sasa hajapiga hatua kimaisha.

MAMA LISHE

Mjasiriamali katika soko hilo la Makoroboi, Madudwa Kafuku, mwenye miaka 20 mahali hapo, anataja mafanikio yake, kama ilivyo kwa muuza viatu, naye amesha-nunua kiwanja cha makazi na anamudu kusomesha wanawe.

Madudwa anasema, hadi sasa ana mgahawa unaomwingizia faida wastani Sh. 10,000 kila kunapokuchwa na ameajiri watumishi wanne anaowalipa kila mmoja Sh.3, 000 kwa siku.

Ana, angalizo kwamba kuna wakati faida inakosekana, lakini amekuwa akivumilia hali hiyo.

KATIBU MACHINGA TAIFA

Katibu Mkuu wa Shirikisho la Umoja wa Machinga Tanzania (SHIUMA) Venatus Anatory, anasema asilimia kubwa ya machinga ni vijana wanaojaribu kuendesha maisha yao kupitia biashara ndogo kama za viatu, nguo na matunda.

Anatory asisitiza kwamba wao machinga wa Mtaa wa Makoroboi, hujikuta wanakinzana na sheria za mipango miji, hata wakafukuzwa kila sehemu, kwa madai ya kuzikiuka.

Hata hivyo, anasema wameshahoji undani kisheria hizo zinazodaiwa kuwazuia wasifanye biashara hasa katikati ya jiji na baadaye waliandaa andiko kuiomba serikali itawatambue rasmi.

Sasa anajivuna, uongozi wa Mama Samia na mtangulizi wake, wamewapatia ruhusa kupitia vitambulisho vya wajasiriamali.

# Ukaguzi ulivyofukua mlolongo wa mashimo ya TEHAMA serikalini

**INATOKA UK. 15**

ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC), Japhet Hasunga, anaishauri serikali kuwekeza kwenye mafunzo kwa wataalamu wa TEHAMA.

"Kuna kitu kilianza kujengeka hivi karibuni kwamba semina nchini ni tatizo, lakini lazima tutambue bila mafunzo na semina kwa wataalamu wetu wa TEHAMA tunatengeneza tatizo kubwa," anatahadharisha.

Ni hoja inayoungwa mkono na mtaalamu wa TEHAMA, pia Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Uwekezaji na Mitaji ya Umma, Atupele Mwakibete, anayeitaka serikali ijipange kuwaimarisha wataalamu nchini kuwa na uwezo wa kukabili uhalifu wa kimataifa mitandaoni.

"Wataalamu wetu wa TEHAMA Ni tatizo, wengi ni wale wa 'copy and paste' (hawana stadi ya ubunifu).

"Serikali ijipange kuhakikisha nchi inakuwa na watalaamu wabobevu ambao wataisaidia nchi kukabiliana na wahalifu wa kimataifa wa mtandaoni," anashauri.

Angalizo la mtaaluma huyo ni kwamba, mifumo inayohifadhi taarifa za TEHAMA zinazotumika (strong backup), hazipo nchini na badala yake ziko nje, huduma hizo zilikonunuliwa.

Ushauri wake ni nini? Mwakibete anayetumia mfano wa madhila yaliyoupata mfumo wa Luku hivi karibuni, anafafanua:

"Mifumo yetu ya TEHAMA kwenye taasisi za serikali na benki zote nchini iwe na 'strong backup' ili kunapotokea tatizo, iwe rahisi kulitatua na kuepuka hasara."

Ofisa kutoka Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA), Sultana Seif, anakiri wamepokea maoni ya CAG na wadau wengine wa TEHAMA, akiahidi watayafanyia kazi.

Anasema hadi sasa wamejipanga kitaifa, wataalamu wa TEHAMA wapatiwe mafunzo walau mara nne kwa mwaka.

# Kenya yaongeza ushuru wa vitunguu, mayai kutoka nje

**Nairobi, KENYA**

KENYA imepitisha sheria inayoongeza tozo katika bidhaa mbalimbali za kilimo zinazoagizwa kutoka nje ya nchi hiyo.

Hatua hiyo inakuja baada ya Rais wa nchi hiyo, Uhuru Kenyatta kusaini muswada wa sheria ya fedha ambayo inaongeza ushuru kwa asilimia 25, kwa mayai na kiasi kama hicho kwa vitunguu vinavyoagizwa kutoka nje. Kenya imekuwa ikiagiza kiasi kikubwa cha mayai na vitunguu kutoka nchi za Tanzania na Uganda, hivyo ongezeko hilo la ushuru huenda likaathiri biashara kati ya nchi hizo za Afrika Mashariki.

Wakati Kenya ikiongeza ushuru kwa bidhaa za kilimo, mataifa ya Afrika yamekuwa yakihimizwa kuondoa vikwazo vya kibiashara, kupitia Mkataba wa Biashara Huru Barani Afrika (AfCFTA), ili kuongeza biashara miongoni mwa nchi hizo.

**BBC**



Wanawafalme William (kushoto) na Harry wakizindua sanamu ya mama yao, Bintimfalme Diana, ikiwa ni kumbukumbu ya miaka 60 ya kuzaliwa mama yao katika bustani ya Sunken, Kasri ya Kensington, jijini London nchini Uingereza juzi. Diana alifariki dunia kwa ajali mwaka 1997, **PICHA: AP**

# Ibada mazishi Kaunda yaanza

**Lusaka, ZAMBIA**

IBADA maalumu ya mazishi ya aliyekuwa rais wa kwanza wa Zambia Kenneth Kaunda, imeanza huku viongozi wa mataifa mbalimbali kutoka barani Afrika na nje ya Afrika wakihudhuria ibada hiyo jijini Lusaka.

Mwaasisi huyo na mpiganiaji uhuru wa taifa la Zambia, alifariki mwezi uliopita akiwa na umri wa miaka 97 kutokana na pneumonia.

Jeshi la Zambia limekuwa likiupitisha mwili wake katika mikoa 10 ya nchi hiyo, ili kuwapa nafasi wananchi kutoa salam zao za mwisho.

Katika hotuba yake hapo jana kwa taifa hilo, Rais wa Zambia Edgar Lungu, alisema ilikuwa mapumziko ili kutoa nafasi kwa wananchi wengi zaidi ushiriki kwenye ibada hiyo, kupitia televisheni.

Ofisi ya Rais wa Afrika Kusini, ilichapisha kwenye mtandao picha ya Rais wa nchi hiyo, Cyril Ramaphosa akisaini kitabu cha rambirambi huko Lusaka.

Kaunda atazikwa Julai 7, mwaka huu, katika maziko ya faragha yatakayohudhuriwa na watu wachache wa familia na viongozi wa juu pekee.

**BBC/RFI**

# WHO: Nchi 16 Afrika zina kirusi Delta

**Geneva, USWISI**

WIMBI la tatu la janga la Covid-19 kirusi cha Delta kinasambaa kwa kasi barani Afrika na mpaka sasa nchi 16 za bara zimebainika kukumbwa na kirusi hicho.

Kwa mujibu wa Shirika la Afya Duniani (WHO), kirusi hicho kinasambaa kwa kasi zaidi barani Afrika, kuliko wakati wowote ikilinganishwa na idadi ya wagonjwa waliobainika wiki iliyopita.

Mkurugenzi wa WHO Kanda ya Afrika, Dk. Matshidiso Moeti alisema, kuongezeka kwa kasi ya kusambaa kwa kirusi hicho kwenye wimbi la tatu la janga la corona ni tishio kwa bara Afrika.

Visa vya wagojwa waliobainika kuwa na virusi vya Delta vimeogezeka zaidi karibu katika wiki sita mfululizo. Kwa mujibu wa takwimu mpya, wimbi hilo la Delta limebainika kwa asilimia 97 na 79 katika nchi ya Jamhuri ya Demokrasi ya Congo (DRC).

Wakati visa vya Delta vikiendelea kuongezeka na watu kulazwa, WHO inakadiria kwamba mahitaji ya oksijen barani Afrika sasa ni asilimia 50 zaidi kuliko ilivyokuwa mwaka jana, lilipoibuka wimbi la kwanza.

**BBC**

# Polisi wadai washambuliaji kupewa mafunzo kigaidi

**Kampala, UGANDA**

POLISI Uganda wamesema watu wenye silaha waliojaribu kumuua waziri, walipatiwa mafunzo katika kambi ya wanamgambo wa kiislamu katika Jamuhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC).

Watu wenye silaha waliokuwa kwenye pikipiki mwezi uliopita walimshambulia kwa bunduki, Waziri wa Kazi na Uchukuzi na Mkuu wa zamani wa Polisi Katumba Wamala, akiwa ndani ya gari lake.

Washukiwa ni sehemu ya kundi lililopewa mafunzo katika kambi moja kwenye jimbo la Kivu Kaskazini, kambi inayoendeshwa na kundi la waasi wa Allied Democratic Forces (ADF), Naibu Mkuu wa Polisi Paul Lokech alisema: ADF linadai kutokuwa na uhusiano na kundi la Islamic State.

Kundi hilo awali lilianzishwa Uganda, ingawa kwa sasa linaendesha operesheni zake katika misitu Mashariki mwa DRC. Jumatatu, washukiwa wawili walishtakiwa kwa kuhusika katika shambulizi hilo, maofisa wa usalama hawakutoa maelezo zaidi ya uchunguzi wao.

**VOA**

# Daraja kupeleka msaada Tigray laharibiwa

**Tigray, ETHIOPIA**

MASHIRIKA ya misaada yameelezea wasiwasi wao kuhusu tatizo la usambazaji misaada ya kiutu, baada ya kuharibiwa kwa daraja muhimu kwenye jimbo la Tigray.

Shirika la Misaada ya Kiutu la International Rescue Committee, limesema kuharibiwa kwa daraja kwenye Mto Tekeze, kutahujumu zaidi juhudi za kupeleka misaada kwenye jimbo la Tigray.

Mkoa huo unaokumbwa na machafuko ni moja ya maeneo yanayokabiliwa na majanga. Marekani ilisema zaidi ya watu 900,000 kwenye mkoa wa Tigray wamekumbwa na baa la njaa.

Haijafahamika wazi ni nani aliyehusika na kubomoa daraja hilo kwenye barabara kuu ya Magharibi mwa Tigray, eneo linalokaliwa na vikosi kutoka jimbo jirani la Amhara. Msemaji wa Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa, Eri Kaneko, alisema pia hali kwenye mji mkuu wa Tigray, Mekelle, bado ni tete.

"Umeme na mawasiliano bado vimekatwa kwenye mkoa huo. Hakuna ndege au barabara ya kuingia au kutoka kwenye eneo hilo."

Mkuu wa Shirika la Misaada ya Maendeleo la Marekani (USAID), Samantha Power alisema kwenye mtandao wake wa Twitter kuwa kuharibiwa kwa daraja hilo ni balaa.

Balozi wa Ufaransa kwenye Umoja wa Mataifa, Nicolas De Riviere, ambaye nchi yake inaongoza Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa, mwezi huu, alisema baraza hilo litaitisha kikao jana, kujadili hali ya kisiasa na ya kiutu kwenye mkoa wa Tigray.

**DW**

# Majeshi Marekani yaondoka Afghanistan baada miongo 2

**Kabul, AFGHANISTAN**

MAMLAKA za Marekani zimedhibitisha, kuondoka kwa wanajeshi wa Marekani, nchini Afghanistan, baada ya kuhudumu nchini kwa kipindi cha miaka 20, wakikabiliana na wapiganaji wa Taliban na kundi la Kigaidi la Al-Qaeda.

Wanajeshi hao wameikabidhi kambi waliyokuwa wakiitumia ya Bagram, kwa wanajeshi wa Afghanstan, huku sherehe ya kurejeshwa rasmi kambi hiyo kwa serikali ya Afghanistan ikitarajiwa kufanyika kesho.

Hata hivyo Kamanda wa Jeshi la Marekani, nchini Afghanistan Jenerali Austin Miller, atasalia Afghanistan, kusaidia wanajeshi kwa muda kabla ya kuondoka.

Hatua ya wanajeshi wa Marekani takriban 2,500 hadi 3,500 kukabidhi kambi yao kwa jeshi la Afghanstan ni ishara kuwa wanaondoka mapema kabla ya kufikia Septemba Mosi, mwaka huu, alivyoahidi Rais Joe Biden.

**VOA**

TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

**NAFASI YA KAZI**

Nafasi za Kazi ya ualimu diploma science na hesabu 0783298900

**Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku**

## KUPOTEA KWA VYETI



**ANITHA ANDENGENYE MWANDISI** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA CHETI CHA KIDATO CHA NNE CHENYE INDEX NAMBA **S1340/0002** KILICHOTOLEWA MWAKA 2006 NA BARAZA LA MITIHANI TANZANIA KUPITIA SHULE YA SEKONDARI LWANGWA,NA CHETI CHA CHUO CHA UALIMU SUMBAWANGA CHENYE NAMBA **E0542/0013** KILICHOTOLEWA MWAKA 2009. YEYOTE ATAKAYEVIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI KILICHO KARIBU.TAARIFA YA POLISI **MBE/MBE/RB/328520/2021**

1163407O2

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

Ndugu **SIIMA SALOME BAKENGESA** anatangaza kupotelewa Kwa kadi yake ya **Gari T 809 ALM.** Kwa yoyote atakaye iona atoe taarifa kituo chochote cha polisi **RB NO. DSM/PHQ/RB/329302/2021.**

116342602

**MAHAKAMA KUU YA TANZANI**
**KANDA YA MBEYA**

**SHAURI LA RUFAA JINAI No. 96 / 2019**

**(Asilia Shauri la Jinai Na.111/2019,Mahakama ya Hakimu Mkazi Mbeya)**

**JAMHURI.......................................................MRUFANI**

**DHIDI YA**

**DAUD DAIMON@MWAKABAJA....................MRUFANIWA**

**KWA : DAUD DAIMON@MWAKABAJA**

**POPOTE MLIPO.**

**KUITWA SHAURINI**

Unaamuriwa na Mahakama hii kuhudhuria hapa Mahakama Kuu Kanda ya Mbeya Tarehe 13/07/2021 siku ya Jumanne saa 03.00 asubuhi bila kukosa,ambapo shauri limepangwa kusikilizwa.
ELEWA KWAMBA,Ukikosa kufika siku hiyo, Shauri litasikilizwa upande mmoja bila WEWE kuwepo na Uamuzi kutolewa.
Hati hii imetolewa kwa amri yangu na Muhuri wa Mahakama hii leo Tarehe 29 Mwezi June, 2021.

NAIBU MSAJILI
MAHAKAMA KUU YA TANZANIA
MBEYA

116342402

**MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**KANDA YA MBEYA**
**SHAURI LA RUFAA JINAI NA. 149 2019**
**(Asilia Shauri la Jinai Na.111/2019, Mahakama ya Hakimu Mkazi Mbeya)**
**JAMHURI.......................................................MRUFANI**
**DHIDI YA**

1. GODGIFT SLAA
2. EDWARD SAMSON CHEM
3. SHABAN RUKWARO MZIRAI........................WARUFANIWA
4. ERNEST MARTIN MGHUNA
5. FRANK MSIGW

**KWA : 1.GODGIFT SLAA**
**2. EDWARD SAMSON CHEM**
**3.SHABAN RUKWARO MZIRAI**
**4.ERNEST MARTIN MGHUNA**
**5.FRANK MSIGWA**

**POPOTE MLIPO.**

**KUITWA SHAURINI**

Unaamuriwa na Mahakama hii kuhudhuria hapa Mahakama Kuu Kanda ya Mbeya Tarehe 13/07/2021 siku ya Jumanne saa 03.00 asubuhi bila kukosa,ambapo shauri limepangwa kusikilizwa.
ELEWA KWAMBA,Ukikosa kufika siku hiyo, Shauri litasikilizwa upande mmoja bila WEWE kuwepo na Uamuzi kutolewa.
Hati hii imetolewa kwa amri yangu na Muhuri wa Mahakama hii leo Tarehe 29 Mwezi June, 2021.

NAIBU MSAJILI
MAHAKAMA KUU YA TANZANIA
MBEYA

116342402

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**MINISTRY OF HOME AFFAIRS**
**IMMIGRATION DIVISION**

**Telegramu: IMMIGRATION**
**Telephone : 027-2751557**
**027-2752284**
**TeleFax 027-275228**
**REF. Na. IMM/MS/DN/16316/VOLI**
**MKUR UGENZI WA MAGAZETI MOSHI**

**THE OFFICE OF THE REGIONAL, IMMIGRATION OFFICER ,**
**P.O.BOX 1049**
**MOSHI**
**KILIMANJARO**
**Date: 30/06/2021**



**HII NI TAARIFA KUWA:**
**BWA GULSHAN KUMAR KEINTH**

Ambaye picha yake imeonyeshwa hapo juu,anaomba uraia kwa Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi .Yeye ni raia wa INDIA na Nchi atokayo ni INDIA.
Kazi yake /Shughuli zake ni Biashara, Anuani ya biashara zake BOX 488 MOSHI
Ameishi nchini tangu 1987, Pia amewahi kuishi Mkoa wa Kilimanjaro tu,
Mtu yeyeto mwenye sababu za kupinga mwombaji asipewe uraia, atume taarifa yake ya maandishi iliyosainiwa kwa:

**KAMISHNA MKUU WA UHAMIAJI,**
**S.L.P 512,**
**DAR ES SALAAM.**

FOR: REGIONAL IMMIGRATION OFFICER

**Kny: AFISA UHAMIAJI MKOA, KILIMANJARO**

116341802

## KUPOTEA KWA CHETI



**JOSEPH PETER** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **P4021/0040** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **YESHUA SEKONDARY SCHOOL** CENTRE mwaka 2014. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **DOD/DOD/RB/328999/2021.**

116341702

## KUPOTEA KWA KADI YA BAJAJI

Ndugu **ANITHA FELICIAN MKUDE** anatangaza kupotelewa Kwa kadi yake ya Bajaji **MC 407 CRF** Kwa yoyote atakaye iona atoe taarifa kituo chochote cha polisi RB NO. **DSM//PHQ/RB/330867/2021.**

116342802

## KUPOTEA KWA KADI YA BAJAJI

Ndugu **SHAFII D MALELKANI** anatangaza kupotelewa Kwa kadi yake ya bajaji (tvs kings) yenye **PLATE NUMBER MC 481 AJT** Kwa yoyote atakaye ona atoe taarifa kituo chochote cha polisi **RB NO. MOR/MOR/RB/293021/2021.**

116340502

## KADI YA BAJAJI IMEPOTEA

**NDG. JACKSON JOHNSON WELLA** Anatangaza kupotelewa na kadi ya BAJAJI yenye namba za usajili **MC 168 BNW - TV KING** rangi ya BLUE. CHASSIS NAMBA: **MD6M14PK9G4K44030.** Atakayeiona anaombwa aripoti kituo chochote cha polisi. Taarifa ya polisi: **MBE/MBE/RB/328691/2021.**

116340602

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**AMINA SILANDA ALLY** ANATANGAZA KUPOTEA KWA KADI YAKE YA GARI YENYE NAMBA ZA USAJILI **T 761 BJQ - MARK X.** CHASSIS NAMBA **GX110034742.** ENGINE NAMBA **106900347.** YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI. TAARIFA YA POLISI: **DAR/OST/RB/328524/2021.**

116341002

## KUPOTEA KWA CHETI



**ROGERS KICHUMU** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S0134-0109** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia MOSHI SEKONDARI mwaka 1994. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **DAR/STA/RB/446379/2019.**

## MNADA WA HADHARA

Kwa idhini tuliyopewa na **TUJIJENGE TANZANIA LTD, SEPCO DEBT COLLECTION & AUCTIONEERING CO. LTD** tunatangaza mnada wa hadhara wa gari lililodhamini mkopo wa mdaiwa Sugu (Magreth Nyambari Nyangwine), gari ni mali ya **FINEST CATHERING SERVICES LIMITED (TOYOTA DYANA -T 994 AYP)** - Gari lipo katika yard ya Makumbusho.
Lengo ni kufidia/ kupunguza deni la mkopo analodaiwa. Mnada utafanyika Tarehe **16/07/2021,** mahali dhamana ilipo. Mteja atalipa 25% siku ya mnada, 75% atalipa ndani ya siku 14 akishindwa kulipa 25% hairudishwi.Gharama za kubadili umiliki ni juu ya mnunuzi.

**Mawasiliano piga:**
**0715683777/0712670704/0713052578**
**Email: info@sepcoauctioneering.co.tz**

116341502

**IN THE HIGH COURT OF TANZANIA**
**SONGEA DISTRICT REGISTRAR**
**AT SONGEA**
**RULE 13, Subordinate Court (Civil Procedure)**

**MIS PC CIVIL APPEAL CASE MATR CAUSES. REV PROB & BILL OF COST NO. .............4/2021**

**ANGELINA CHOWO.........................DECREE HOLDER**

**VERSUS**

**BLANDINA MGIMBA..................DECREE DEBTOR**

**TO: BLANDINA MGIMBA**

**NOTICE OF DATE MENTION**

**TAKE NOTES** that the above case has been fixed for Mention on 22 day of JULY 2021 at 09.00 a.m
Before Hon **M.A. MALEWO DR.**
You are required to appear in this Court without fail any and you Must produce on that day all the documents upon which you intend. To reply in support of your case.
Given under my hand and the seal of Court this **16th day of JUNE of 2021**

DEPUTY REGISTRAR

**TO BE SERVED UP ON:**

**BLANDINA MGIMBA**

116341602

**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**

**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**

**Katika Mahakama ya Mwanzo MJINI MOROGORO**

**Usimamizi wa Mirathi NO.196/2021**

**Ombi la REHEMA MOHAMED ABDALLAH Kuteuliwa Msimamizi wa Mirathi ya Marehemu TULIA SAID MUHANGO**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaalikwa kuja kuhudhuria shaurini mnamo tarehe 23/07/2021 kabla huyo mwambaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
Wosia wa marehemu huyo upo hapa mahakamani waweza kukaguliwa. Tarehe 01/07/2021

HAKIMU
MAHAKAMA YA MWANZO MJINI
MOROGORO

116342502

**MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**KANDA YA MWANZA**
**SHAURI LA MADAI NO 10 YA MWANZA 2021**
**MKOMBOZI COMMERCIAL BANK PLC.........MDAI**
**DHIDI YA**
**JOSEPH RICHARD MASOLWA................MDAIWA**

**Kwa: JOSEPH RICHARD MASOLWA**

**KUITWA SHAURINI**

Unaarifiwa kuhudhuria hapa mahakamani tarehe 19/07/2021 kuja kusikiliza shauri la madai lililofunguliwa na mdai dhidi yako.
Unaarifiwa kufika bila kukosa wewe au wakili wako, kutofika kwako shauri hili litasikilizwa upande mmoja dhidi yako na kutolewa maamuzi.
Hati hii imetolewa kwa mkono wangu na chapa ya mahakama leo tarehe 29/06/2021.

NAIBU MSAJILI
MAHAKAM KUU TANZANIA
MWANZA

116342902

**OFISI ZA MATANGAZO**
**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# HADITHI

TOM alipooa alidhani kuwa ataishi kwa amani, furaha na kupata utulivu kama inavyokuwa kwa rafiki na wenzake wote waliofanya hivyo.


Siku zote ndoa ni masikilizano, maelewano, na anayeoa hupata furaha na heshima. Kinyume chake, kwake imekuwa ni misukosuko, mikosi na balaa. Badala ya kuwa ndoa yenye furaha, akajiingiza kwenye mtego hatari ambao hata baada ya kuufahamu, hakuweza kuutegua tena. Alichelewa. Ukawa ni mwanzo ni vilio, maafa na mtiririko wa mambo ya kushangaza.

Hebu pata kila nakala ya gazeti hili kufuatilia kisa hiki cha kushangaza na kusikitisha.

# Namsaka mke wangu-1

**Mtunzi anapatikana (0716 350534)**

**Na Adam Fungamwango**




MACHOZI ya kiume yalimtoka. Alidhani labda anaota, lakini haikuwa hivyo. Yote yaliyotokea ni kweli tupu. Akarudisha kumbukumbu ya wiki moja tu iliyopita.

Alikuwa kwenye hoteli moja ya kifahari katikati ya Dar es Salaam, iliitwayo Paradiso. Umati wa watu ulikula na kunywa. Watu walikuwa na kusaza. Anakumbuka aliitwa na MC yeye na mkewe Farida kwenda kusakata dansi. Alikuwa anajua kucheza. Hata mwenyewe alilijua hilo. Hakutegemea kuwa mkewe Farida pia alikuwa anajua mno kulisakata.

Walicheza kwa ustadi mkubwa. Ilikuwa ni kama walikuwa wameufanyia mazoezi wimbo huo. Staili zote walicheza sawa. Shangwe lililopigwa hapo halikuwa la kitoto. Watu walishangilia na kuwatunza pesa lukuki.

Hiyo ilikuwa ni usiku. Kabla ya hapo alifunga ndoa kwenye Kanisa la Chang'ombe. Tayari alikuwa mkewe.

Ilikuwa ni moja kati ya siku za kukumbukwa sana kwenye maisha yake. Wiki moja baadaye yote yamefutika.

"Kwa nini? Kwa nini Farida wangu. Nini kimetokea? Mbona mapema hivi? Nitamwambia nani mimi? Nitalia na nani mimi?"

Pamoja na kwamba alipenda sana Farida na anaona hawezi kuishi bila yeye, kingine kilichomliza zaidi na zaidi na atаanzaje kuwaambia watu kuwa mkewe hayupo tena nyumbani?

Atawezaje kuwaambia kuwa mkewe ametoroka? "Ndiyo ametoroka." Alijiambia. Hilo alikuwa ana uhakika nalo.

Angeweza kudhani labda mkewe amepotea. Angeweza kwenda kuripoti kwenye kituo cha polisi Chang'ombe na kupewa RB ya kupotelewa na mkewe.

Angedhani hivyo kama bi harusi asingeacha ujumbe. Huo ndiyo uliomfanya aone kuwa ameondoka makusudi. Kwa kifupi ametoroka.

Tomas Sanze kila akifikiria umati uliokuwa kwenye harusi yake, michango na jinsi ilivyofana, ni kama kichaa kilitaka kutaka kumpanda.

"Nitawaambia nini watu hawa? Mbona Farida umeniletea aibu mimi? Ni nini? Kwa nini hukukataa mapema kuolewa na mimi ili aibu hii isinikute?" Alijuta.

Akili ikamtuma kuwa kabla ya kuwaambia watu kuwa bi harusi aliyemuona wiki moja tu iliyopita, kiasi kwamba hata nje alikuwa hajaanza kutoka, na piko aliyopaka bado haijakauka, ametoroka.

Alikiangalia tena kile kikaratasi kilichoandikwa na bi harusi. Alikisoma tena. Hii ilikuwa ni zaidi ya mara 20. Siyo kama hakuwa anaelewa, ila hakuwa anaamini kile kilichoandikwa. Alikisoma tena na tena, kana kwamba kuna wakati atakuta maandishi yamebadilika. Lakini kila anapokisoma yale maneno yalionekana kama kumsisitizia kile kilichoandikwa "Nimeondoka na usinitafute."

Kila akifikiria mawazo yake yanafika sehemu yanagota. Hakujua ni nini kimempata. "Amewehuka ghafla?" Alijiuliza. Lakini akajijibu kuwa angewehuka asingeweza kuandika alichokiandika.

Pamoja na yote hayo, Tom alitambua kama si mzaha, basi lipo tatizo kubwa lililopo kwa mkewe.

Kwanza kabisa alikumbuka kuwa suala la kuolewa lilisisitizwa sana mkewe Farida na si yeye. Kwa upande wake alitaka ndoa ifungwe mwezi Desemba. Lakini akasitiza kuwa ifungwe haraka. Leo hii wiki moja tu mke ameondoka. Ametoroka. Tena ameandika waraka mfupi tu kuwa ameondoka na asitafutwe.

"Nitakosaje kukutafuta wakati wewe ni mke wangu Farida? Umekwenda wapi? Kufanya nini? Oooh Farida wangu, nakupenda sana. Kwa nini umenifanyia hivi?"

Kingine kilichomchanganya na kushangaza ni upendo mkubwa alionao kwake. Kwa muda wa mwaka mmoja alioishi naye kama mchumba hakuwa na shaka kuwa Farida anampenda sana yeye.

"Kitu gani kimembadilisha?" Hakujua.

Baada ya kujiuliza kila swali, kujijibu, kuchanganua yake anayoweza kuyachangua. Mwisho akajikuta akipata wazo moja tu. Kumtafuta. Kumsaka mkewe.

"Nitaanzia wapi?" Hilo ndiyo swali la kwanza baada ya maamuzi yake. Ndiyo kwa sababu kwa ndugu zake wote Dar es Salam alipiga simu na kuambiwa hawajamuona. Kila anapopiga majibu ni yale yale. Siyo simu tu. Tom alidhani kuwa huenda ndugu zake hasa wa Dar wanamdanganya. Akaamua kuwa atakwenda huko huko kwao, sehemu moja baada ya nyingine na kuwahoji kwa kina kiasi kwamba akapata uhakika kuwa hajafika hapo.

Pamoja na kwamba alipenda sana kuishi kwa dada yake Kigamboni Mikwambe na huko ndiko taratibu za posa na kila kitu zilifanyikia, lakini aliishi zaidi Morogoro maeneo ya Kichangani.

**Kila akifikiria mawazo yake yanafika sehemu yanagota. Hakujua ni nini kimempata. "Amewehuka ghafla?" Alijiuliza. Lakini akajijibu kuwa angewehuka asingeweza kuandika alichokiandika.**

Licha ya kwamba nako alifanya nao mawasiliano na kuambiwa nako hajaonekana, lakini alitaka aende kama alivyofanya kwa ndugu wengine ili apate uhakika wa asilimia zote.

Ni yeye pekee ndiye aliyeonekana kutumia nguvu kubwa kumpata kuliko ndugu wa bi harusi. Alijua sababu yake. Ni kwamba wanajua hayupo sehemu hatarishi. Mtu anayeandika kuwa anaondoka ni kwamba anajua anakokwenda. Kama asingeandika chochote, hata ndugu wangeungana naye kumsaka Farida. Hata yeye alijua hajapotea. Hajakufa. Na wala hayupo kwenye sehemu hatari.

Anachojuliza tu ni kwamba "Yupo kwa nani? Kwa nini? Na kwa nini iwe hivyo wakati yeye tayari ni mke wa mtu?" Alijua mtu anayepotea na ndugu zake wanakuwa na wasiwasi sana ni yule ambaye anapotea ghafla na hakuna taarifa yoyote kuwa yupo wapi.

Kila kitu kilikuwa moyoni mwa Tom. Wasiwasi, hasira, wivu vilimchoma

"Nitakwenda Morogoro. Nitakwenda kusaka mke wangu." Alisema akizuidi kufuta machozi akiwa peke yake varandani kwenye sofa.

**ITAENDELEA JUMAMOSI**



# NUNO KUAMUA KUHUSU KANE

**LONDON,** England

KOCHA mpya wa Tottenham Hotspur, Nuno Espirito Santo, ametaarifiwa kwamba atakuwa na neno la mwisho kama Harry Kane aruhusiwe kuondoka au la kipindi hiki cha majira ya joto.

Kane amekuwa akihusishwa na mpango wa kuondoka pale Spurs huku majaliwa yake yakiwa kwenye sintofahamu.

Straika huyo awali alibainisha kwamba, anataka kuondoka klabuni hapo kipindi hiki cha majira ya joto kwa ajili ya kutafuta changamoto nyingine.

Lakini baada ya kuwasili kwa kocha mpya, Santo sasa yeye ndiye mwenye neno la mwisho la kumruhusu aondoke au kumpigania abakie hapo.

Hata hivyo, inaamini kwamba, nahodha huyo wa England hajakuwa kwenye mazungumzo yoyote na klabu yake hiyo katika wiki za hivi karibuni, huku akiwa na timu ya taifa kwenye michuano ya Euro 2020.

Gazeti la Telegraph limeripoti kwamba, Mwenyekiti wa Spurs, Daniel Levy amesisitiza kuwa hatamuuza straika wake huyo bila ushauri kutoka kwa kocha wake mpya, Espirito Santo.

Kwa maana hiyo, ushauri wa kocha huyo wa zamani wa Wolves ndio utakaotoa hatima ya Kane kama auzwe au abakie klabuni hapo.

# Sancho kukamilisa usajili baada ya Euro 2020

**MANCHESTER.** England

MANCHESTER United imethibitisha kufikia makubaliano ya muhimu ya kumsajili, Jadon Sancho, ambaye anakamilisha uhamisho huo baada ya michuano ya Euro 2020.

Sancho anatarajiwa kuwa mchezaji wa nne kusajiliwa kwa bei ghali zaidi katika hitoria ya United nyuma ya Paul Pogba, Harry Maguire na Romelu Lukaku, baada ya miamba hao wa Ligi Kuu England kukubali kulipa euro milioni 85 kutoka Borussia Dortmund.

United ilikuwa inawania kumsajili mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 21 kwa muda mrefu, lakini hawakufanikiwa kwa wakati huo, huku Dortmund walikuwa hawana malengo ya kumuuza.

Hata hivyo, klabu hiyo ya Ligi Kuu ya Ujerumani, Bundesliga, ilithibitisha kuwa Alhamisi ilifikia makubaliano ya kumuuza winga huyo ambaye alitua hapo akitokea Manchester City.

Na sasa mashetani wekundu hao watakamilisha uhamisho wake baada ya michuano ya euro 2020.

"Manchester United inafuraha kutangaza kwamba, imefikia makubaliano muhimu na Borussia Dortmund kwa ajili ya kumsajili Jadon Sancho," taarifa fupi ya Man United ilisomeka.

"Usajili wake unakamilika mara baada ya kufanyiwa vipimo vya afya yake baada ya michuano ya Euro 220."





# *White azigonganisha Arsenal, Brighton*

**LONDON,** England

ARSENSAL inakabiliwa na ushindani mkubwa kutoka kwa Everton katika harakazi zao za kutaka kumsajili mlinzi wa kati wa Brighton na England, Ben White.

Toffees hao kwa sasa wakiwa chini ya kocha, Rafa Benitez wameingiza kwenye soko la usajili kwa ajili ya kuimarisha kikosi chao tayari kwa msimu mpya.

Washikabunduki hao wanakaribia kumsajili mchezaji huyo, lakini Brighton wametia mguu kwenye mbio za kuwania saini yake.

Brighton walikataa ofa ya pauni milioni 40 kutoka Arsenal mapema mwezi uliopita na Daily Mail liliripoti kuwa ofa ya pili ya pauni milioni 42 na nyongeza ya pauni milioni 6 pia ilikataliwa.

Klabu hiyo inataka pauni milioni 50 kwa ajili ya kumuachia mchezaji huyo na Everton wameanza mazungumzo yao wiki hii.

Imeripotiwa kuwa Everton bado hawajatuma ofa yao, lakini imewaarifu Brighton kuwa italipa kiasi kikubwa kuliko kile kilichotolewa na Arsenal.

Everton majuzi ilitangaza kumteua ramsi kocha wa zamani wa Liverpool kuwa kocha wao mpya na amesaini mkataba wa miaka mitatu.

## HABARI MICHEZO

# Juventus wajipanga kumuuza Ronaldo

**TURIN,** Italia

JUVENTUS wapo tayari kumuuza Cristiano Ronaldo kwa pauni milioni 25 kipindi hiki cha majira ya joto wakati wakiangalia uwezekano wa kumuachia nyota huyo wa Ureno.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 36 alitua hapo Turin mwaka 2018 akitokea Real Madrid, baada ya kupata mafanikio makubwa nchini England na Hispania.

Huku mchango wake wa mabao umekuwa muhimu zaidi kwa timu hiyo, akifunga mabao 101 katika mechi 133 alizocheza na sasa Juve wanapanga kumuuza.

Gazzetta dello Sport limeripoti kuwa Juve ipo tayari kumuachia raia huyo wa Ureno kwa kiasi hicho cha fedha wakati huu wa dirisha la usajili wa kipindi cha majira joto.

Klabu yake ya zamani ya Manchester United na Real Madrid pamoja na miamba wa Ligi Kuu ya Ufaransa, Paris Saint-Germain, wameripotiwa kumuwania fowadi huyo.

Ingawa mkurugenzi wa soka wa Juve, Federico Cherubini hivi karibuni alisema hatarajii kumuona akiondoka kipindi hiki cha majira ya joto, lakini ni wazi kwamba, Ronaldo sasa yupo njiani kuondoka.





# RAMOS AKARIBIA KUSAINI PSG

**PARIS,** Ufaransa

KLABU ya Paris Saint-Germain ipo kwenye nafasi nzuri ya kushinda mbio za kumsajili Sergio Ramos kwa uhamisho huru, baada ya mkataba wake kumalizika kule Real Madrid Jumatano, alikocheza kwa kipindi cha miaka 16.

PSG sasa inatajwa kwamba inakaribia kufikia makubaliano ya kumsajili mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 35, huku timu kama Manchester City na Bayern Munich zikiwania saini yake.

Kwa mujibu wa ESPN, Ramos na miamba hao wa Ligue 1 wapo kwenye hatua nzuri ya kufikia 'makubaliano ya awali', ili kufikia uamuzi ya mwisho.

Mchezaji huyo ambaye aliachwa kwenye kikosi cha Hispania kinachoshiriki michuano ya Euro 2020 anataka mkataba wa miaka miwili wa kucheza na klabu yoyote itakayofikia makubaliano ya kumsajili.

Taarifa za awali zilipasha kwamba, wao PSG wanaweza kuwa tayari kukubali masharti ya Ramos.

# Varane hana haraka na hatima yake

**MANCHESTER,** England

PAPHAEL Varane hatakuwa na haraka ya kufanya uamuzi kuhusu majaliwa yake, akiwa amechukua likizo baada ya kutolewa kwenye michuano ya Euro 2020 na akiwa amefanya majadiliano na kocha mpya wa Real Madrid, Carlo Ancelotti kabla ya kuamua uhamisho wake.

Varane ambaye ni mlinzi wa kati anawaniwa zaidi na Manchester United kipindi hiki cha majira ya joto, ingawa hakuna majadiliano binafsi yaliyofikiwa kati ya klabu hiyo na mchezaji.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 28 alibainisha mapema mwezi uliopita kwamba anapanga kuondoka Real Madrid kwa ajili ya kutafuta changamoto mpya.

Klabu za Chelsea na Paris Saint-Germain zimekuwa zikihusishwa nae, lakini United ndio wanaopewa nafasi kubwa zaidi ya kupata saini yake.

Iliripotiwa mapema Alhamisi kwamba, dili hilo linakaribia kukamilika, lakini bado hakujawa na taarifa zozote rasmi.

Hata hivyo, gazeti la L'Equipe limeripoti kwamba, Varane kwa sasa anaangalia majaliwa yake na wapi atakapocheza msimu ujao.

Ingawa taarifa zaidi zinasema kwamba anasubiria kwanza kukutana na Ancelotti kujadiliana nae hatima yake.



# DONDOO SOKA MAGAZETI ULAYA




# XAVI: BARCA, MESSI WANAHITAJIANA

●●● Asema kama ingekuwa kubeti, basi angembetia abaki lakini...

**BARCELONA,** Hispania

LIONEL Messi alikuwa mchezaji huru Alhamisi, lakini Xavi anaamini ni suala la muda tu kabla ya nahodha huyo mwenye rekodi ya ufungaji mabao kusaini mkataba mpya hapo Barcelona.

**Wakati kwa sasa akiwa na kikosi cha Argentina kwenye michuano ya Copa America 2020, Messi amejielekeza zaidi kwenye mashindano hayo na hata wakati Julai ilipoingia hakuwa na neno lolote kuhusu mkataba mpya pale Camp Nou.**

Hiyo inamaana kwamba, mkataba wake umeshamalizika na kumfanya Messi kuwa huru kusajiliwa na timu yoyote ili kumsajili.

Amekuwa akihusishwa na mpango wa kutakiwa na Manchester City na Paris Saint-Germain na kumekuwa na minong'ono kwamba, Messi amekubali kubakia Barcelona.

Mchezaji mwenzake wa zamani, Xavi anahisi Messi anakaribia kusaini mkataba mpya na miamba hao wa Katalunya na wana nafasi nzuri ya kumpa mkataba mpya nyota huyo mwenye umri wa miaka 34.

"Hili ni suala na soko, tunatakiwa kusubiri," alisema Xavi. "Tunaamini anazungumza na klabu na rais.

"Namtakia kila la heri Leo, kama rafiki na mtu wangu wa karibu ambaye tumekuwa pamoja pale Barcelona.

"Nataka yeye aendelee kuwa hapa Barca. Matumaini yangu inaweza kutangazwa wakati wowote inavyowezekana."

Akizungumza na Mundo Deportivo, Xavi, ambaye kwa sasa ni kocha wa Al Sadd, aliongeza: "Kama ningetakiwa kubeti, ningesema kwamba, ataendelea kuwa klabuni hapa, ingawa mambo mengi yamezungumzwa, lakini ningependa yeye aendelee kucheza hapa.

"Leo anaihitaji Barca na Barca inamhitaji Leo. Yeye ana furaha kuwa hapa Barcelona; amecheza kwa maisha yake yote hapa. Ningeweza kubeti kwamba anaweza kusaini mkataba mpya."

## ZISIKUPITE

### RAMOS HUYO PSG

KLABU ya Paris St-Germain ipo katika mazungumzo yaliopiga hatua ili kumsajili beki wa Hispania, Sergio Ramos, 35, kwa uhamisho huru, baada ya kumaliza muda wake wa kucheza Real Madrid. ***(ESPN)***

### CALVERT-LEWIN KUTUA MAN

MANCHESTER United inafikiria kumsajili mshambuliaji wa England na Everton, Dominic Calvert-Lewin, 24. ***(Sun)***

### RICE AIKATAA WEST HAM

KIUNGO wa kati wa England, Declan Rice, 22, amekataa ofa mbili za kandarasi kutoka West Ham, huku akitajwa kuwaniwa na Chelsea , Manchester united na Manchester City ***(Guardian)***

### NUNO NA KANE

KOCHA mpya wa klabu ya Tottenham Hotspur, Nuno Espirito Santo ameambiwa nahodha Harry Kane, 27, hatauzwa bila ya baraka zake, ingawa mshambuliaji huyo wa England anatarajiwa kuelezea mpango wake wa kuondoka katika klabu hiyo. ***(Telegraph - subscription required)***

### WHITE ANUKIA EVERTON

EVERTON inatumai kuishinda Arsenal katika usajili wa beki wa Brighton, Ben White, 23, huku maombi mawili ya washikabunduki hao tayari yamekataliwa na beki huyo wa kati wa England. ***(Mail)***

### BARCA KUMUUZA FIRPO

BARCELONA inatumaini kukamilisha mauzo ya beki wa Hispania, Junior Firpo, 24 kwa Leeds United katika siku chache zijazo na pia inapanga kumuuza kwa mkopo Miralem Pjani. ***(Sport)***

### LIVER YAMTAKA GRAVENBERCH

LIVERPOOL inamchunguza kiungo wa kati wa Brighton na Mali, Yves Bissouma mbali na mchezaji wa Ajax na Uholanzi, Ryan Gravenberch, 19, huku wakitaka kuziba pengo lililoachwa wazi na Georginio Wijnaldum, ambaye alijiunga na PSG mapema wakati wa dirisha la uhamisho. ***(Liverpool Echo)***

### SPURS KUMSAJILI COADY

KLABU ya Tottenham Hostpur inatarajiwa kushindana na Everton katika jaribio la kumsaijili beki wa England, Conor Coady kutoka Wolves. ***(Football Insider)***

### TAMIYASU KUSAJILIWA SPURS

TOTTENHAM Hotspur pia imeipatia Bologna euro milioni 15 pamoja na gharama nyingine kwa beki wa Japan, Takehiro Tomiyasu, 22, ambaye amemvutia nia kutoka kwa Manchester United na Atalanta. ***(Athletic)***

### WILLIAN KUUZWA

ARSENAL inafikiria kumuuza Willian, 32, msimu huu, lakini mahitaji ya winga huyo wa Brazil hayawavutii wanaomtaka. ***(Football London)***

## Mirambo ataka mikoa kuratibu kozi za makocha

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

MKURUGENZI wa Ufundi Shirikisho la mpira wa miguu Tanzania, TFF, Oscar Mirambo ametoa wito kwa mikoa yote ambayo haijaendesha mafunzo ya makocha kufanya hivyo.

Mirambo alitoa wito huo jana mjini Kibaha baada ya kushiriki mafunzo ya kozi ya Diploma D ya CAF kozi ya awali ya kimataifa iliyoandaliwa na chama Cha walimu wa mpira wa miguu mkoa wa Pwani.

Alisema kufanyika kwa kozi hizo kutawafanya wahitaji wengi kunufaika na kuondokana na kusafiri umbali mrefu kwenda mikoa mingine kupata elimu hiyo.

"Matamanio yangu kozi hii ifanyike mikoa yote hapa nchini na hapa natoa wito kwa kila mkoa kufanya hivyo, waratibu na waombe kibali TFF ili waweze kuendesha na wanaohitaji wanufaike," alisema Mirambo.

Mwenyekiti wa chama cha walimu wa mpira wa miguu mkoa wa Pwani, Riziki Majala, alisema kozi hiyo imefanyika kwa ushirikiano wa TFF, Ofisi ya mkuu wa shule ya Sekondari Kibaha na washiriki ambao walitoa michango itakayowezesha kupata huduma mbalimbali za chakula.

Washiriki wa mafunzo hayo wametoka mikoa ya Geita, Mtwara, Tanga Dar es salam, na wenyeji Pwani.

## Fainali kombe la ZFF kupigwa Julai 5

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

FAINALI ya Michuano ya kombe la Shirikisho la Zanzibar, ZFF, inatarajiwa kupigwa keshokutwa Jumatatu ya Julai 5.

Mgeni rasmi katika hatua ya Fainali anatarajiwa kuwa Waziri wa habari, Vijana Sanaa na Michezo ,Tabia Maulid Mwita, ambapo mechi hizo zitapigwa uwanja wa Amaan.

Nusu fainali ya kwanza ilipigwa jana Ijumaa kati ya KVZ dhidi ya Polisi huku fainali ya pili inachezwa leo Jumamosi kati ya KMKM dhidi ya Mafunzo.

Akizungumza na gazeti hili Mratibu wa michuano hiyo, Haji Issa Kidali alisema maandalizi yote ya kuelekea hatua ya fainali yamekamilika.

Alisema kuwa katika msimu huu michuano hiyo imechezwa katika Kanda ya Unguja pekee ambapo bingwa ataiwakilisha Zanzibar katika michuano ya Kombe la Shirikisho Barani Africa, CAF.

Kwa mujibu wa kanuni ya ZFF kwa msimu wa 2020-2021, endapo timu ya KMKM ambayo ndio Bingwa wa ligi kuu ya Zanzibar ikifanikiwa kutwaa ubigwa wa Kombe hilo la FA, basi Mshindi wa Pili wa ligi kuu ya Zanzibar ndio ataiwakilisha Zanzibar katika kombe la Shirikisho.

# KAGERA YAJIPANGA KUPATA POINTI SITA

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Kagera Sugar, Francis Baraza, anazipigia hesabu mechi zao mbili za mwisho za Ligi Kuu Tanzania bara ili kuhakikisha anapata pointi sita.

**Kagera imebakiza mechi dhidi ya Polisi Tanzania itakayochezwa Julai 14, uwanja wa Ushirika Moshi na dhidi ya Coastal Union mkoani Tanga.**

Akizungumza na gazeti hili jana, Baraza alisema mipango yake ni kufanya vizuri kwenye mechi hizo mbili zilizosalia akipigania kushinda na kuvuna pointi sita.

"Ligi imekuwa tamu na chungu mno, kila timu kuanzia juu mpaka chini ni vita, hakuna urahisi kwa mechi zetu zote zilizosalia, tumefanya vizuri kwenye mechi mbili za nyumbani na kutoka katika nafasi ya 13 hadi 12," alisema Baraza.

"Tunahitaji pointi sita, nina imani wachezaji wakijituma tunaweza kupata pointi muhimu katika hizo mechi za ugenini na kujiweka katika nafasi nzuri ya kushiriki ligi kuu msimu ujao."

Alisema kila mechi kwao ni mapambano ya kutafuta matokeo chanya na imani na wachezaji wake, kufanya yale anayowapa kwenye mazoezi na kuonyesha uwanjani katika mechi kuhakikisha wanapambana katika michezo hiyo kutafuta pointi hizo.

Kagera wako nafasi ya 12 na kukusanya pointi 37 na anahitaji pointi sita ili kujiweka katika nafasi nzuri ya kuendelea kucheza ligi hiyo.




Katibu Mkuu wa Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), Wilfred Kidao, akimkabidhi tuzo ya Mchezaji Bora wa Ligi Daraja la Kwanza ya Wanawake (WFDL) 2021, Jacqueline Joseph wa Ilala Queens, katika fainali ya michuano hiyo iliyofanyika juzi jijini Dodoma. Kushoto ni Kaimu Mwenyekiti wa Chama cha Mpira wa Miguu cha Wanawake Nchini (TWFA), Somoe Ng'itu na kulia ni Mkurugenzi wa Shule za Fountain Gate, Japhet Makau. **NA MPIGAPICHA WETU**



# *Ali Kiba apagawisha mashabiki Buza*

**Na Sabato Kasika**

MSANII wa muziki wa kizazi kipya, Ali Kiba, ameonyesha kuwa ana uwezo mkubwa katika muziki huo baada ya kuibua shangwe na nderemo za mashabiki alipotumbuiza katika kilele cha onyesho la siku ya vibonzo.

Kilele cha onyesho hilo kilifanyika kwenye uwanja wa michezo wa 'Business' eneo la Buza kwa Mama Kibonge jijini Dar es Salaam juzi na kuhudhuriwa na wasanii mbalimbali wakiwamo wachanga.

Msanii huyo alipanda jukwaani akiwa na kundi lake la madansa sambamba na mdogo wake Abdul Kiba na kuimba baadhi ya nyimbo zake zikiwamo za 'Salute na Ndombolo ya Solo na kuibua shangwe za mashabiki.

Wakongwe wengine waliopanda jukwaani ni Chegge Chigunda kutoka TMK , huku akifuatiwa na mkongwe wa dansi Mwinjuma Muumin aliyetumbuiza kwa wimbo wake mpya wa 'Kwa Mpalange'.

Aidha, burudani nyingine zilizojiri ni pamoja na kinyang'anyiro cha kumpata Miss Buza ambapo taji lilikwenda kwa Amina Abdallah na pia wasanii mbalimbali wazawa wa eneo hilo la Buza walipata nafasi ya kutoa burudani.

# Michezo

Jumamosi Julai 3, 2021

Nipashe






Xavi: Barca, Messi wanahitajiana UKURASA 22




# SIMBA, YANGA SC MWISHO WA UBISHI

## ●●● Wekundu watamba kutangaza ubingwa, Wanajangwani wasema wako...

**Na Mandishi Wetu**

WATANI wa jadi katika soka ya Tanzania, Simba na Yanga leo wanashuka dimbani kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam, katika mchezo wa pili wa Ligi Kuu ya Tanzania Bara, ambao unatarajiwa kupigwa kuanzia saa 11:00 jioni.

**Simba ni mabingwa watetezi na kinara wa ligi hiyo, itakuwa nyumbani na kushuka dimbani wakiwa na kumbukumbu ya kutoka sare ya bao 1-1, mchezo wa mzunguko wa kwanza dhidi ya Yanga ambao walikuwa wenyeji.**

Timu hizo mbili zikinolewa na makocha huku Simba ikiwa chini ya Mfaransa, Didier Gomes na Yanga chini ya Nasreddine Nabi raia wa Tunisia.

Kocha Nabi tayari amewaweka kando mastaa watatu wa kigeni, Haruna Niyonzima, beki na nahodha Lamine Moro na mshambuliaji Michael Sarpong kwa madai ya utovu wa nidhamu.

Simba nao wataendelea kukosa huduma ya kiungo wao Jonas Mkude ambaye alipelekwa kwenye kamati ya nidhamu ambayo ilishauri nyota huyo kupelekwa hospitali kulingana na utovu wake wa nidhamu kujirudia mara kwa mara.

Wakizungumza wa waandishi wa habari jijini jana, Simba iliwakilishwa na Kocha Msaidizi, Selemani Matola na Yanga ikiwakilishwa na Razak Siwa, kila mmoja alioa tambo zake.

Matola alisema kuwa mchezo huo utakuwa mgumu na ushindani mkubwa, na wanawaheshimu Yanga na wanaenda uwanjani kwa ajili ya kusaka pointi tatu ili kutangaza ubingwa.

Kwa upande wa Siwa alisema wamejiandaa kwenda kushinda kwa sababu wamefanyia kazi upungufu wa timu yao ikiwamo nafasi ya kipa.

### TAKWIMU

Mpaka wanakwenda kukutana leo hii Simba na Yanga wameshakutana mara 105 tangu mwaka 1965, hivyo leo zinakutana kwa mara ya 106.

Kwa mujibu wa takwimu zilizopo za watani hao, katika mechi hizo 105, Yanga imeshinda mara 37, Simba ikiwa imepata ushindi mara 31.

Timu hizo zimetoka sare mara 37, Yanga ikifunga mabao 150, Simba ikiwa na mabao 136. Ni mechi 43 ambazo Yanga haikuruhusu bao, huku Simba ikicheza mechi 32 kati ya 105 bila kuruhusu bao.

### KAULI YA POLISI

Kamanda wa Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam, Jumanne Muliro (pichani), jana aliwahakikishia usalama wananchi wote watakaokwenda kutazama mechi hiyo kwenye Uwanja Mkapa.



Alisema: "Jeshi la Polisi tumejipanga vyema kuhakikisha mashabiki, viongozi na wachezaji wanakuwa salama, lakini pia ulinzi ndani na nje ya uwanja."

***Imeeandikwa na Saada Akida, Adam Fungamwango na Sophia Mwilawa.***

## UCHAGUZI TFF:
# Korti Kuu yaruhusu mchakato uendelee

**Na Kulwa Mzee**

MAHAKAMA Kuu imeruhusu mchakato wa uchaguzi wa Rais wa Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania (TFF) kuendelea ikiwamo maandalizi na kampeni wakati kesi ya msingi ya kupinga uchaguzi huo kutokana na kasoro zilizopo kwenye Katiba ikiendelea.

Uamuzi huo ulitolewa jana na Jaji Edwin Kakolaki baada ya kupitia hoja za pande zote mbili zinazopingana.

"Mlalamikaji anaomba zuio la muda la mchakato wa uchaguzi, katika hati yake ya kiapo alishindwa kuishawishi mahakama kukubali maombi yake.

"Hakuonesha madhara yanayoweza kutokea endapo mchakato huo ukiendelea," alisema Jaji Kakolaki.

Alisema kutokana na hoja hiyo, maombi ya zuio yamekataliwa na kwamba wajibu maombi watawasilisha majibu ya madai ya mlalamikaji Julai 6 na mlalamikaji atawasilisha majibu kama yapo Julai 8, mwaka huu na kesi itaanza kusikilizwa Julai 9, mwaka.

Mawakili katika maombi hayo walivutana vikali, mlalamikaji akitaka zuio huku walalamikiwa wakiomba mchakato uendelee. Mlalamikaji katika shauri hilo ni Ally Salehe na mlalamikiwa ni Bodi ya Wadhamini ya TFF, TFF na Mwenyekiti Kamati ya Uchaguzi.

Wakili wa Mlalamikaji, Frank Chacha, aliiomba mahakama kukubali maombi ya kusimamisha mchakato wote wa uchaguzi huo kwa muda wakisubiri usikilizwaji wa kesi ya msingi ya kusimamisha uchaguzi huo.

Alidai endapo kampeni zitaendelea na masuala yote yanayohusiana na uchaguzi yakiendelea, ikiwamo gharama zinazotumika wakati kuna maombi ya zuio mahakamani, maombi yao yatakuwa hayana msingi kuwapo.

"Ninaomba mahakama itoe amri ya kuzuia mchakato mzima unaohusu uchaguzi wakati wakisubiri pande zote mbili kusikilizwa," alidai Chacha.

Wakili Chacha alidai Mahakama isipotoa zuio, serikali itapata hasara ya fedha, pia itasababisha hasara kwa mlalamikaji.

Katika hati ya kiapo, mlalamikaji Ally anadai kuwapo ubaguzi katika Katiba ya TFF kuhusiana na uchaguzi.

Anadai kwa mujibu wa Katiba, mgombea urais anatakiwa kuidhinishwa na wajumbe wa kamati tendaji watano wakati Zanzibar hakuna wajumbe wa kamati hiyo.

Wakili wa walalamikiwa, Alex Muchunguzi, akiwasilisha hoja, alidai maombi walipewa juzi jioni hivyo wanahitaji muda wa kuwasilisha majibu.

Aliomba mahakama ikubali mchakato kuhusiana na uchaguzi ikiwamo kampeni ziendelee wakati maombi yakisikilizwa.

Katika maombi, Ally anaomba mahakama iwazuie walalamikiwa kufanya uchaguzi Agosti 7, mwaka huu kama ilivyotangazwa Juni 8, mwaka huu.


GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 9

9 770856 541002 >